New Hampshire
**Department of Education**

# Mwongozo wa Ulinzi wa Kisheria wa Elimu Maalum

**Novemba 2023**

New Hampshire Department of Education
25 Hall Street, Concord, NH 03301

# Notisi ya Ulinzi wa Kisheria
## wa Sehemu ya B ya Sheria

Sheria ya Elimu ya Watu wenye Ulemavu (Individuals with Disabilities Education Act (IDEA)), sheria ya Shirikisho kuhusu elimu ya wanafunzi wenye ulemavu, inahitaji shule ziwapatie nyinyi, wazazi wa mtoto mwenye ulemavu, notisi iliyo na maelezo kamili ya ulinzi wa kisheria unaopatikana chini ya sheria ya IDEA na kanuni za Idara ya Elimu ya Marekani (U.S Department of Education). **Ni lazima upewe nakala ya notisi hii mara moja tu kwa mwaka wa shule**, **isipokuwa katika hali zifuatazo:**

(1) baada ya rufaa ya kwanza au ukiomba tathmini;

(2) baada ya kupokea lalamiko lako la kwanza la Jimbo chini ya 34 CFR §§300.151 hadi 300.153 na baada ya kupokea lalamiko lako la kwanza la mchakato wa haki chini ya §300.507 katika mwaka wa shule;

(3) wakati uamuzi unafanywa kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mtoto wako ambazo zinajumuisha mabadiliko ya uwekaji; na

(4) kwa ombi lako. [34 CFR §300.504(a)]

**U.S. Department of Education**
Office of Special Education and Rehabilitative Services,
Office of Special Education Programs

## Utangulizi

Watoto wana uwezekano mkubwa wa kufanikiwa wakati wazazi na walimu wanashirikiana pamoja ili kubuni na kufikia malengo ya kielimu kwa watoto wenye ulemavu. Sheria ya Shirikisho na Jimbo hutoa fursa nyingi kwa wazazi kushiriki katika kupanga na kufanya maamuzi kuhusu mahitaji ya elimu maalum ya mtoto wao.

Mwongozo huu umeundwa kuwapa wazazi, wanafunzi watu wazima wenye ulemavu, walimu na wengine habari kuhusu haki za mzazi/mtoto katika mchakato wa kutoa elimu maalum. Haki hizi zinaitwa "ulinzi wa kisheria."

Timu ya IEP hubaini tathmini, ustahiki, Mpango wa Elimu Binafsi (Individualized Education Program (IEP)), na uwekaji wa kielimu wa mtoto. Jina rasmi la Timu hii ni Timu ya IEP, lakini inaweza kurejelewa kwa majina mengine kulingana na kazi au shughuli inayoangaziwa. Timu ya IEP ni kikundi ambacho hufanya maamuzi mengi makubwa kuhusu mahitaji na huduma za elimu maalum za mtoto.

Wazazi ni washirika kamili wa Timu ya IEP; maoni ya mzazi ni muhimu na yanahitaji kujumuishwa. Mchakato wa kutoa elimu maalum huwapa wazazi fursa ya kushiriki maarifa na ujuzi wao kuhusu mtoto wao na wengine kwenye Timu ya mtoto wao. Sheria hii ilianzishwa ili kutoa fursa kwa wazazi kushiriki katika mchakato wa elimu maalum na kukuza mawasiliano kati ya shule na wazazi kwa niaba ya mtoto wao. Mchakato wa elimu maalum huwa na ufanisi zaidi wakati wazazi na wafanyakazi wa shule wana habari za kutosha na wanaweza kushirikiana pamoja.

Ni muhimu hasa kwa wazazi na wengine wanaohusika katika mchakato wa elimu maalum kuelewa haki zao na kufahamu kuhusu sheria za vikomo vya muda na vikwazo vingine ili kupata elimu ya bure na inayofaa ya umma (FAPE).

# Msaada/Raslimali za Bila Malipo au za Gharama Nafuu

| | | |
|---|---|---|
| **Parent Information Center (PIC)**<br>54 Old Suncook Road<br>Concord, New Hampshire 03301<br>(603) 224-7005 au 1-800-947-7005<br>www.picnh.org | **Disabilities Right Center, Inc.**<br>P.O. Box 3660<br>Concord, New Hampshire 03301<br>Simu: (603) 228-0432<br>au 1-800-834-1721<br>Barua pepe:<br>advocacy@drcnh.org<br>www.drcnh.org | **Bureau of Special Education, New Hampshire Department of Education**<br>25 Hall Street<br>Concord, New Hampshire 03301<br>Simu: (603) 271-3741 |

Tafadhali kumbuka kuwa ingawa mwongozo huu unakidhi masharti chini ya *Sheria ya Elimu ya Watu wenye Ulemavu ya 2004 (Individuals with Disabilities Education Act of 2004 (IDEA 2004))* kwamba wazazi wapewe hati iliyoandikwa ambayo inaelezea ulinzi wa kisheria ambao wana haki wa kupata, haujumuishi maandishi yote ya sheria au kanuni za elimu maalum za Shirikisho au Jimbo.

# Muhtasari wa Mchakato wa Elimu Maalum wa New Hampshire

Mchakato wa elimu maalum unajumuisha hatua mahususi, kila moja ikiwa na masharti yake. Kila hatua katika mchakato wa elimu maalum inajumuisha taratibu zinazotumika kwako na wilaya ya shule kushirikiana pamoja. Utaratibu wa mchakato wa elimu maalum ni:

**Utambuzi/Kupata Mtoto**
NH Ed 1105

↓

**Rufaa**
NH Ed 1106

↓

**Tathmini**
NH Ed 1107

↓

**Ubainishaji wa Ustahiki**
NH Ed 1108

↓

**Kubuniwa na Kuidhinishwa kwa Mpango wa Elimu Binafsi (IEP)**
NH Ed 1109

↓

**Uwekaji**
NH Ed 1111

↓

**Ufuatiliaji na Ukaguzi wa IEP wa Kila Mwaka**
NH Ed 1109.06

*Kumbuka: Baadhi ya mikutano hii inayohitajika inaweza kuunganishwa. Kwa maelezo zaidi kuhusu hatua zilizo katika mchakato, angalia sheria zilizorejelewa au tembelea www.picnh.org.*

# Orodha ya Yaliyomo


**Maelezo ya Jumla ........ 1**
- Notisi ya Awali Iliyoandkiwa ........ 1
- Lugha ya Asili ........ 2
- Barua ya Kielektroniki ........ 2
- Idhini ya Mzazi—Ufafanuzi ........ 3
- Idhini ya Mzazi ........ 3
- Tathmini Huru za Kielimu ........ 7

**Usiri wa Taarifa ........ 9**
- Ufafanuzi ........ 9
- Taarifa Binafsi Zinazoweza Kutambulisha Mtu ........ 9
- Notisi kwa Wazazi ........ 9
- Haki za Ufikiaji ........ 10
- Rekodi ya Ufikiaji ........ 10
- Rekodi za Zaidi ya Mtoto Mmoja ........ 11
- Orodha ya Aina na Maeneo ya Taarifa ........ 11
- Ada ........ 11
- Marekebisho ya Rekodi Yanayoombwa na Mzazi ........ 11
- Fursa ya Usikilizaji wa Kesi ........ 12
- Utaratibu wa Usikilizaji wa Kesi ........ 12
- Matokeo ya Usikilizaji wa Kesi ........ 12
- Idhini ya Kufichua Taarifa Binafsi Zinazoweza Kutambulisha Mtu ........ 12
- Ulinzi wa Kisheria ........ 13
- Kuharibiwa kwa Taarifa ........ 13

**Utaratibu wa Lalamiko la Jimbo ........ 14**
- Tofauti Kati ya Taratibu za Malalamiko na Kesi za Mchakato wa Haki na Malalamiko ya Jimbo ........ 14
- Kupitishwa kwa Taratibu za Lalamiko la Jimbo ........ 14
- Muda wa Chini Zaidi wa Taratibu za Lalamiko la Jimbo ........ 15
- Kuwasilisha Lalamiko la Jimbo ........ 16

**Taratibu za Lalamiko la Mchakato wa Haki ........ 18**
- Kuwasilisha Lalamiko la Mchakato wa Haki ........ 18
- Lalamiko la Mchakato wa Haki ........ 18
- Upatanisho ........ 20

Mchakato wa Utatuzi ........ 22

**Usikilizaji wa Kesi za Malalamiko ya Mchakato wa Haki ........ 25**
Usikilizaji Kesi Usio na Upendeleo wa Mchakato wa Haki ........ 25
Haki ya Usikilizaji wa Kesi ........ 27
Maamuzi ya Usikilizaji wa Kesi ........ 28

**Rufaa ........ 29**
Uamuzi wa Mwisho; Rufaa; Ukaguzi Usio na Upendeleo ........ 29
Ratiba na Ufaafu wa Usikilizaji wa Kesi na Ukaguzi ........ 30
Kesi za Kiraia, Ikiwa ni Pamoja na Kipindi cha Muda cha Kuwasilisha Kesi Hizo ........ 30
Uwekaji wa Mtoto Wakati Lalamiko na Usikilizaji wa Kesi wa Mchakato wa Haki Unasubiriwa ........ 32
Ada za Mawakili ........ 33

**Taratibu Wakati wa Kuwaadhibu Watoto Wenye Ulemavu ........ 35**
Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule ........ 35
Mabadiliko ya Uwekaji kwa Sababu ya Uondoaji wa Kinidhamu ........ 38
Ubainishaji wa Mazingira ........ 39
Rufaa ........ 39
Uwekaji Wakati wa Rufaa ........ 40
Ulinzi kwa Watoto ambao Bado Hawajastahiki Elimu Maalum na Huduma Zinazohusiana ........ 40
Rufaa kwa na Hatua za Mamlaka za Utekelezaji wa Sheria na Mahakama ........ 42

**Masharti ya Uamuzi wa Wazazi wa Kuweka Watoto katika Shule za Kibinafsi kwa Gharama ya Serikali ........ 43**
Jumla ........ 43

# MAELEZO YA JUMLA

## NOTISI ya Awali Iliyoandikwa

## 34 CFR §300.503, NH Ed 1120.03

### Notisi

Wilaya yako ya shule lazima ikupe notisi iliyoandikwa (kukupa maelezo fulani kwa maandishi), siku 14 za kalenda kabla ya wilaya:

1. Kupendekeza kuanzisha au kubadilisha utambuzi, tathmini, au uwekaji wa elimu wa mtoto wako, au utoaji wa elimu ya bure na inayofaa ya umma (FAPE) kwa mtoto wako; **au**
2. Kukataa kuanzisha au kubadilisha utambuzi, tathmini, au uwekaji wa elimu wa mtoto wako, au utoaji wa FAPE kwa mtoto wako.

### Yaliyomo kwenye notisi

Notisi iliyoandikwa lazima:

1. Ieleze hatua ambayo wilaya yako ya shule inapendekeza au inakataa kuchukua;
2. Ieleze kwa nini wilaya yako ya shule inapendekeza au kukataa kuchukua hatua;
3. Ieleze kila utaratibu wa tathmini, ukadiriaji, rekodi, au ripoti ambayo wilaya yako ya shule ilitumia kuamua kupendekeza au kukataa hatua hiyo;
4. Ijumuishe taarifa kwamba una ulinzi chini ya masharti ya ulinzi wa kisheria katika Sehemu ya B ya sheria ya IDEA;
5. Ikueleze jinsi unaweza kupata maelezo ya ulinzi wa kisheria ikiwa hatua ambayo wilaya yako ya shule inapendekeza au kukataa sio rufaa ya kwanza ya tathmini;
6. Ijumuishe huduma za usaidizi za kuwasiliana nazo kwa msaada wa kuelewa Sehemu ya B ya sheria ya IDEA;
7. Ieleze machaguo mengine yoyote ambayo Timu ya Mpango wa Elimu Binafsi (IEP) ya mtoto wako ilizingatia na sababu kwa nini machaguo hayo yalikataliwa; **na**
8. Itoe maelezo ya sababu zingine kwa nini wilaya yako ya shule ilipendekeza au kukataa hatua hiyo.

### Notisi kwa lugha inayoeleweka

Notisi lazima iwe:

1. Imeandikwa kwa lugha inayoeleweka kwa umma; **na**
2. Imetolewa katika lugha yako ya asili au njia nyingine ya mawasiliano unayotumia, isipokuwa ikiwa haiwezekani kufanya hivyo.

Ikiwa lugha yako ya asili au njia nyingine ya mawasiliano sio lugha iliyoandikwa, wilaya yako ya shule lazima ihakikishe kuwa:

1. Notisi imefasiriwa kwako kwa kutamkwa au kwa njia nyingine katika lugha yako ya asili au njia nyingine ya mawasiliano;
2. Unaelewa maudhui yaliyomo kwenye notisi; **na**
3. Kuna ushahidi ulioandikwa kwamba masharti yaliyo katika aya ya 1 na 2 yametimizwa.

# LUGHA YA ASILI

## 34 CFR §300.29

*Lugha ya asili,* inapotumiwa kwa mtu ambaye ana ujuzi mdogo wa Kiingereza, inamaanisha yafuatayo:

1. Lugha ambayo kwa kawaida hutumiwa na mtu huyo, au, ikiwa ni mtoto, lugha ambayo kwa kawaida hutumiwa na wazazi wa mtoto;
2. Katika mawasiliano yote ya moja kwa moja na mtoto (ikiwa ni pamoja na tathmini ya mtoto), lugha ambayo kawaida hutumiwa na mtoto nyumbani au katika mazingira ya masomo.

Kwa mtu mwenye uziwi au upofu, au kwa mtu asiyetumia lugha ya maandishi, njia ya mawasiliano ni njia ambayo mtu huyo kawaida hutumia (kama vile lugha ya ishara, Breli, au mawasiliano ya kutamka).

# BARUA YA KIELEKTRONIKI

## 34 CFR §300.505

Ikiwa wilaya yako ya shule inawapa wazazi chaguo la kupokea hati kwa barua pepe, unaweza kuchagua kupokea hati zifuatazo kwa barua pepe:

1. Notisi ya Awali Iliyoandikwa;
2. Notisi ya ulinzi wa kisheria; **na**
3. Notisi zinazohusiana na lalamiko la mchakato wa haki.

# IDHINI YA MZAZI - UFAFANUZI

## 34 CFR §300.9

### Idhini

*Idhini* inamaanisha:

1. Umearifiwa kikamilifu katika lugha yako ya asili au njia nyingine ya mawasiliano (kama vile lugha ya ishara, Breli au mawasiliano ya kutamka) maelezo yote kuhusu hatua ambayo unatoa idhini kuhusu.

2. Unaelewa na unakubaliana kwa maandishi na hatua hiyo, na idhini inaelezea hatua hiyo na inaorodhesha rekodi (ikiwa zipo) ambazo zitatolewa na kwa nani; **na**
3. Unaelewa kuwa idhini ni ya hiari kwa upande wako na kwamba unaweza kuondoa idhini yako wakati wowote.

Ikiwa unataka kubatilisha (kughairi) idhini yako baada ya mtoto wako kuanza kupokea elimu maalum na huduma zinazohusiana, lazima ufanye hivyo kwa maandishi. Uondoaji wako wa idhini hautangui (kutendua) kitendo ambacho kimefanyika baada ya kutoa idhini yako lakini kabla ya kuiondoa. Aidha, wilaya ya shule haihitajiki kurekebisha (kubadilisha) rekodi za elimu za mtoto wako ili kuondoa marejeleo yoyote kwamba mtoto wako alipokea elimu maalum na huduma zinazohusiana baada yako kuondoa idhini.

#### Uhamisho wa Haki

Kwa mujibu wa Ed 1120.01, 34 CFR 300.320(c), na 34 CFR 300.520, uhamisho wa haki za ulezi hutokea mwanafunzi anapofikisha umri wa miaka 18, isipokuwa wazazi wa mwanafunzi wamebaki na haki ya ulezi kupitia uamuzi wa mahakama.

## IDHINI YA MZAZI

### 34 CFR §300.300, NH Ed 1120.04

#### Idhini ya tathmini ya kwanza

Wilaya yako ya shule haiwezi kufanya tathmini ya kwanza kwa mtoto wako ili kubaini ikiwa mtoto wako anastahiki chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA kupokea elimu maalum na huduma zinazohusiana bila kwanza kukupa notisi ya maandishi ya hatua inayopendekezwa na kupata idhini yako kama ilivyoelezwa chini ya vichwa vya ***Notisi ya Awali Iliyoandikwa*** na ***Idhini ya Mzazi.***

Wilaya yako ya shule lazima ifanye juhudi za kutosha kupata idhini yako ya ufahamu kwa tathmini ya kwanza ili kubaini ikiwa mtoto wako ni mtoto mwenye ulemavu.

Idhini yako kwa tathmini ya kwanza haimaanishi kuwa pia umetoa idhini yako kwa wilaya ya shule kuanza kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mtoto wako.

Wilaya yako ya shule haipaswi kutumia hatua yako ya kukataa kuidhinisha huduma au shughuli moja inayohusiana na tathmini ya kwanza kama msingi wa kukunyima wewe au mtoto wako huduma, usaidizi au shughuli nyingine yoyote, isipokuwa masharti mengine ya Sehemu ya B yanaihitaji wilaya ya shule kufanya hivyo.

Ikiwa mtoto wako ameandikishwa katika shule ya umma au unanuia kumwandikisha mtoto wako katika shule ya umma na umekataa kutoa idhini au umekosa kujibu ombi la kutoa idhini ya tathmini ya kwanza, wilaya yako ya shule inaweza, lakini haihitajiki, kufanya tathmini ya kwanza ya mtoto wako kwa kutumia upatanisho chini ya sheria ya IDEA au malalamiko ya mchakato wa haki, mkutano wa utatuzi, na taratibu za usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki usio na upendeleo. Wilaya yako ya shule haitakiuka majukumu yake ya kupata, kutambua na kutathmini mtoto wako ikiwa haitafanya tathmini kwa mtoto wako katika hali hizi.

Wazazi wa watoto wenye ulemavu watakuwa na siku 14 baada ya kutumwa kwa notisi ya awali iliyoandikwa ili kusaini hati hiyo kuashiria idhini, kukataa idhini au kuidhinisha kwa sehemu.

### Idhini ya mzazi kwa huduma

Wilaya yako ya shule lazima ipate idhini yako ya ufahamu kabla ya kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mtoto wako kwa mara ya kwanza.

Wilaya ya shule lazima ifanye juhudi za kutosha kupata idhini yako ya ufahamu kabla ya kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mtoto wako kwa mara ya kwanza.

Ukikosa kujibu ombi la kutoa idhini yako kwa mtoto wako kupokea elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza, au ukikataa kutoa idhini hiyo au baadaye ubatilishe (ughairi) idhini yako kwa maandishi, wilaya yako ya shule haipaswi kutumia ulinzi wa haki (yaani, upatanisho, lalamiko la mchakato wa haki, mkutano wa utatuzi au usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki usio na upendeleo) ili kufikia makubaliano au uamuzi kwamba elimu maalum na huduma zinazohusiana (zinazopendekezwa na Timu ya IEP ya mtoto wako) zinaweza kutolewa kwa mtoto wako bila idhini yako.

Ukikataa kutoa idhini yako kwa mtoto wako kupokea elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza, au ukikosa kujibu ombi la kutoa idhini hiyo au baadaye ubatilishe (ughairi) idhini yako kwa maandishi na wilaya ya shule ikose kutoa kwa mtoto wako elimu maalum na huduma zinazohusiana ambazo ilitafuta idhini yako kutoa, wilaya yako ya shule:

1. Haitakuwa imekiuka masharti ya kutoa elimu ya bure na inayofaa ya umma (FAPE) kwa mtoto wako kwa kutotoa huduma kwa mtoto wako; **na**
2. Haihitajiki kufanya mkutano wa mpango wa elimu binafsi (IEP) au kuunda IEP ya mtoto wako kwa elimu maalum na huduma zinazohusiana ambazo idhini yako iliombwa.

Ukibatilisha (ukighairi) idhini yako kwa maandishi wakati wowote baada ya mtoto wako kuanza kupata elimu maalum na huduma zinazohusiana, basi wilaya ya shule inapaswa kuacha kutoa huduma hizo, lakini lazima ikupe notisi ya awali iliyoandikwa, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa cha ***Notisi ya Awali Iliyoandikwa***, kabla ya kusitisha huduma hizo.

### Idhini ya mzazi kwa tathmini mpya

Wilaya yako ya shule lazima ipate idhini yako ya ufahamu kabla ya kutathmini upya mtoto wako, isipokuwa kama wilaya yako ya shule inaweza kuthibitisha kwamba:

1. Ilichukua hatua za kutosha kupata idhini yako kwa tathmini mpya ya mtoto wako; **na**
2. Hukujibu.

Ikiwa utakataa kukubali tathmini mpya ya mtoto wako, wilaya ya shule inaweza, lakini haihitajiki, kutafuta kibali cha kufanya tathmini ya mtoto wako kwa kutumia upatanisho, malalamiko ya mchakato wa haki, mkutano wa utatuzi, na taratibu za usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki usio na upendeleo ili kuchukua hatua kinyume na hatua yako ya kukataa kukubali tathmini mpya kwa mtoto wako. Kama ilivyo kwa tathmini za kwanza, wilaya yako ya shule haitakuwa imekiuka majukumu yake chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA ikiwa itakataa kutafuta kibali cha kufanya tathmini mpya kwa njia hii.

Kwa tathmini mpya, mchakato, kama ilivyoelezwa katika Ed 1102.02 (n), utakamilika ndani ya siku 60 baada ya kupokea idhini ya mzazi ya kufanya tathmini. Baada ya idhini ya maandishi ya wahusika wote, kikomo cha muda wa siku 60 kinaweza kuongezwa kwa idadi mahususi ya siku, bila kuzidi siku 30.

### Hati za juhudi za kutosha za kupata idhini ya mzazi

Shule yako lazima ihifadhi hati za juhudi za kutosha za kupata idhini yako ya kufanya tathmini ya kwanza, kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza, kwa ajili ya tathmini mpya, na ili kupata wazazi wa watoto katika Jimbo kwa tathmini za kwanza. Hati lazima zijumuishe rekodi ya majaribio ya wilaya ya shule katika maeneo haya, kama vile:

1. Rekodi za kina za simu zilizopigwa au kujaribiwa na matokeo ya simu hizo; **na**
2. Nakala za barua za mawasiliano zilizotumwa kwako na majibu yoyote yaliyopokewa.

### Idhini ya Kudokezwa

Kwa mujibu wa Ed 1120.06, ikiwa mzazi atakosa kujibu ndani ya siku 14 baada ya kutumwa kwa notisi ya awali iliyoandikwa, wilaya itatekeleza mabadiliko yaliyopendekezwa ikiwa imefanya juhudi za kutosha kupata idhini ya maandishi.

Juhudi za kutosha zitajumuisha:

- Kumbukumbu za simu zilizopigwa au kujaribiwa kwa mzazi na matokeo ya simu hizo; **na**
- Nakala za barua za mawasiliano zilizotumwa kwa mzazi na majibu yoyote yaliyopokewa. Barua za mawasiliano zitatumwa kwa barua iliyothibitishwa, na risiti ya kuthibitisha uwasilishaji itaombwa.

### Masharti mengine ya idhini

Idhini yako haihitajiki kabla ya wilaya yako ya shule kuweza:

1. Kukagua data iliyopo kama sehemu ya tathmini au tathmini mpya ya mtoto wako; **au**
2. Kumpa mtoto wako mtihani au tathmini nyingine ambayo hutolewa kwa watoto wote isipokuwa, kabla ya mtihani au tathmini hiyo, idhini inahitajika kutoka kwa wazazi wa watoto wote.

Ikiwa umeandikisha mtoto wako katika shule ya kibinafsi kwa gharama yako mwenyewe au ikiwa unamsomesha mtoto wako nyumbani, na ukatae kutoa idhini yako kwa tathmini ya kwanza ya mtoto wako au tathmini mpya ya mtoto wako, au ukose kujibu ombi la kutoa idhini yako, wilaya ya shule haipaswi kutumia taratibu zake za utatuzi wa mgogoro (yaani, upatanisho, lalamiko la mchakato wa haki, mkutano wa utatuzi, au usikilizaji wa kesi wa mchakato wa haki usio na upendeleo) na haihitajiki kuzingatia mtoto wako kama anayestahiki kupokea huduma sawa (huduma zinazopatikana kwa watoto wengine wa shule ya kibinafsi walio na ulemavu waliowekwa katika shule hiyo na wazazi wao).

**Udhuru kwa Mkutano wa Washirika wa Timu**

Shirika la Elimu la Eneo (LEA) au mzazi ataarifu mhusika huyo mwingine kuhusu kutoweza kuwepo kwa mshirika wa timu angalau saa 72 kabla ya mkutano uliopangwa au baada ya kufahamu kuwa anatarajia kutokuwepo, yoyote inayokuja kwanza kulingana na Ed 1103.01 (e).

Mzazi lazima aidhinishe udhuru huo kwa maandishi ikiwa mshirika ni mshirika anayehitajika wa Timu ya IEP kulingana na 34 CFR 300.321.

**Kanuni maalum kwa tathmini ya kwanza ya watoto walio chini ya ulezi wa Jimbo**

Ikiwa mtoto ni mtoto aliye chini ya ulezi wa Jimbo na haishi na mzazi wake —

Wilaya ya shule haihitaji idhini kutoka kwa mzazi kwa tathmini ya kwanza ili kubaini ikiwa mtoto ni mtoto mwenye ulemavu ikiwa:

1. Licha ya juhudi za kutosha kufanya hivyo, wilaya ya shule haiwezi kumpata mzazi wa mtoto huyo;

2. Haki za wazazi zimekomeshwa kwa mujibu wa sheria za Jimbo; **au**

3. Hakimu amempa mtu mwingine ambaye si mzazi haki ya kufanya maamuzi ya kielimu na mtu huyo ametoa idhini ya tathmini ya kwanza.

**Wazazi Mbadala wa Uwakilishi wa Kielimu**
NH Ed 1115

Ikiwa mtoto mwenye ulemavu anahitaji elimu maalum na mzazi au mlezi hajulikani au hawezi kupatikana baada ya juhudi za kutosha kufanywa ili kumpata mzazi huyo, au ikiwa mtoto yuko chini ya ulinzi wa kisheria wa kitengo cha watoto, vijana, na familia, kamishna au mwakilishi wake anaweza kuteua mzazi mbadala ambaye atawakilisha mtoto katika mchakato wa kufanya maamuzi ya kielimu.

**Uwakilishi Katika Kufanya Maamuzi**

Kwa mujibu wa RSA 186-C:3-c, ikiwa mlezi wa mtu mzima anajadiliwa na Timu ya IEP pamoja na mwanafunzi na familia ya mwanafunzi, timu itajulisha mwanafunzi na familia kuhusu upatikanaji wa uwakilishi wa kufanya maamuzi kama mbadala wa walezi. Hii itafanywa mara moja ulezi unapojadiliwa kwa mara ya kwanza. Timu ya IEP itatoa huduma za msaada ili kusaidia kuhakikisha makubaliano ya kufanya uwakilishi wa kufanya maamuzi yanafanywa. Timu ya IEP itazingatia maamuzi yaliyofanywa na mwanafunzi kulingana na makubaliano.

# TATHMINI HURU ZA KIELIMU

## 34 CFR §300.502, NH Ed 1107.03

### Jumla

Kama ilivyoelezwa hapo chini, una haki ya kupata tathmini huru ya elimu (IEE) ya mtoto wako ikiwa hukubaliani na tathmini ya mtoto wako ambayo ilifanywa na wilaya yako ya shule.

Ukiomba tathmini huru ya elimu, wilaya ya shule lazima ikupe habari kuhusu mahali unakoweza kupata tathmini hiyo huru ya elimu na kuhusu vigezo vya wilaya ya shule vinavyotumika kwa tathmini huru za elimu.

### Ufafanuzi

*Tathmini huru ya elimu* inamaanisha tathmini inayofanywa na mchunguzi aliyehitimu ambaye hajaajiriwa na wilaya ya shule inayohusika katika elimu ya mtoto wako.

*Gharama ya serikali* inamaanisha kuwa ama wilaya ya shule inalipia gharama kamili ya tathmini au inahakikisha kuwa tathmini inatolewa vinginevyo bila wewe kulipishwa, kulingana na masharti ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, ambayo yanaruhusu kila Jimbo kutumia vyanzo vyovyote vya Jimbo, vya eneo, Shirikisho, na vya kibinafsi vya msaada vinavyopatikana katika Jimbo ili kukidhi masharti ya Sehemu ya B ya sheria hii.

### Haki ya kupata tathmini inayolipiwa na serikali

Una haki ya kupata tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya serikali ikiwa hukubaliani na tathmini ya mtoto wako iliyofanywa na wilaya yako ya shule, kulingana na hali zifuatazo:

1. Ikiwa unaomba tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya serikali, wilaya yako ya shule lazima, bila kuchelewa kusikohitajika, <u>ama</u>: (a) Iwasilishe lalamiko la mchakato wa haki ili kuomba usikilizaji wa kesi ili kuthibitisha kuwa tathmini yake ya mtoto wako inafaa; <u>au</u> (b) Ifanye tathmini huru ya elimu kwa gharama ya serikali, isipokuwa wilaya ya shule ikithibitisha katika usikilizaji wa kesi kwamba tathmini ya mtoto wako ambayo umepata haikukidhi vigezo vya wilaya ya shule.
2. Wilaya yako ya shule ikiomba usikilizaji wa kesi na uamuzi wa mwisho ni kwamba tathmini ya wilaya yako ya shule inamfaa mtoto wako, bado una haki ya kupata tathmini huru ya elimu, lakini sio kwa gharama ya serikali.
3. Ukiomba tathmini huru ya elimu ya mtoto wako, wilaya ya shule inaweza kukuuliza kwa nini unapinga tathmini ya mtoto wako iliyofanywa na wilaya yako ya shule. Hata hivyo, huenda wilaya yako ya shule isihitaji ufafanuzi na haipaswi kuchelewesha bila sababu inayofaa ama kutoa tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya serikali au kuwasilisha lalamiko la mchakato wa haki ili kuomba usikilizaji wa kesi wa mchakato wa haki ili kutetea tathmini ya wilaya ya shule ya mtoto wako.

Una haki ya kupata tathmini moja tu huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya serikali kila wakati wilaya yako ya shule inapomfanyia mtoto wako tathmini ambayo hukubaliani nayo.

### Tathmini zinazoanzishwa na mzazi

Ikiwa utapata tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya serikali au ushiriki na wilaya ya shule tathmini ya mtoto wako ambayo ulifanyiwa kwa gharama yako binafsi:

1. Wilaya yako ya shule lazima izingatie matokeo ya tathmini ya mtoto wako, ikiwa inakidhi vigezo vya wilaya ya shule vya tathmini huru za elimu, katika uamuzi wowote unaofanywa kuhusiana na utoaji wa elimu ya bure na inayofaa ya umma (FAPE) kwa mtoto wako; **na**
2. Wewe au wilaya yako ya shule inaweza kuwasilisha tathmini kama ushahidi katika usikilizaji kesi ya mchakato wa haki kuhusu mtoto wako.

### Maombi ya tathmini na hakimu

Ikiwa hakimu anaomba tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kama sehemu ya usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki, gharama ya tathmini lazima ilipiwe na serikali.

### Vigezo vya wilaya ya shule

Ikiwa tathmini huru ya elimu inalipiwa na serikali, vigezo ambavyo tathmini itafanywa, ikiwa ni pamoja na eneo la tathmini na sifa za mchunguzi, lazima viwe sawa na vigezo ambavyo wilaya ya shule hutumia wakati inaanzisha tathmini (kwa kiwango ambacho vigezo hivyo vinaendana na haki yako ya kupata tathmini huru ya elimu).

Isipokuwa kwa vigezo vilivyoelezwa hapo juu, wilaya ya shule haipaswi kuweka masharti au ratiba ya muda inayohusiana na kupata tathmini huru ya elimu inayolipiwa na serikali.

# USIRI WA TAARIFA

## UFAFANUZI

### 34 CFR §300.611, NH Ed 1115

- *Uharibifu* unamaanisha uharibifu halisi au kuondolewa kwa vitambulishi vya binafsi kutoka kwa taarifa ili taarifa hiyo isiweze kutambulisha mtu tena.
- *Rekodi za elimu* zinamaanisha aina ya rekodi zilizobainishwa chini ya ufafanuzi wa ‘‘rekodi za elimu’’ katika 34 CFR Sehemu ya 99 (kanuni zinazotekeleza Sheria ya Haki za Elimu za Familia na Faragha ya 1974, 20 U.S.C. 1232g (FERPA)).
- *Shirika linaloshiriki* linamaanisha wilaya ya shule, shirika au taasisi yoyote inayokusanya, kuhifadhi, au kutumia taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha mtu, au shirika ambako taarifa inapatikana, chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA.

## TAARIFA BINAFSI ZINAZOWEZA KUTAMBULISHA MTU

### 34 CFR §300.32

*Taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha mtu* zinamaanisha taarifa zinazojumuisha:

(a) Jina la mtoto wako, jina lako kama mzazi, au jina la mwanafamilia mwingine;

(b) Anwani ya mtoto wako;

(c) Kitambulishi cha binafsi, kama vile nambari ya ustawi wa jamii au nambari ya mwanafunzi ya mtoto wako; **<u>au</u>**

(d) Orodha ya sifa za kibinafsi au taarifa zingine ambazo zitawezesha kutambua mtoto wako kwa uhakika wa kutosha.

## NOTISI KWA WAZAZI

### 34 CFR § 300.612

New Hampshire Department of Education au mashirika mengine ya jimbo yanaweza pia kupata, kuhifadhi au kutumia rekodi za shule. Mashirika haya lazima yafuate masharti ya kulinda usiri au taarifa zozote binafsi zinazoweza kutambulisha mtu walizohifadhi kuhusu mtoto (Tazama 34 CFR 300.612 kwa maelezo zaidi) ikiwa ni pamoja na:

1. Maelezo ya kiwango ambacho notisi hutolewa katika lugha za asili za vikundi mbalimbali vya watu katika Jimbo;
2. Maelezo ya watoto ambao taarifa zao binafsi zinazoweza kuwatambulisha zinahifadhiwa, aina ya taarifa zinazotafutwa, mbinu ambazo Jimbo linatarajia kutumia katika kukusanya taarifa hizo (ikiwa ni pamoja na vyanzo ambavyo taarifa hizo hukusanywa kutoka kwake), na matumizi ya taarifa hizo;

3. Muhtasari wa sera na taratibu ambazo mashirika yanayoshiriki lazima yafuate kuhusu uhifadhi, ufichuaji wa taarifa kwa wahusika wengine, uwekaji, na uharibifu wa taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha mtu; **na**
4. Maelezo ya haki zote za wazazi na watoto kuhusu taarifa hizi, ikiwa ni pamoja na haki chini ya Sheria ya Haki za Elimu za Familia na Faragha (Family Educational Rights and Privacy Act (FERPA)) na kanuni zake za utekelezaji katika 34 CFR Sehemu ya 99.

Kabla ya shughuli yoyote kubwa ya kutambua, kupata, au kutathmini watoto wanaohitaji elimu maalum na huduma zinazohusiana (pia inajulikana kama "kupata mtoto"), notisi lazima ichapishwe au itangazwe katika magazeti au vyombo vingine vya habari, au vyote viwili, na taarifa za kutosha zitolewe ili kuwajulisha wazazi katika Jimbo kuhusu shughuli hizi.

# Haki ya Ufikiaji

## 34 CFR §300.613, New Hampshire RSA 189:66

Shirika linaloshiriki lazima likuruhusu uangalie na ukague rekodi zozote za elimu zinazohusiana na mtoto wako zinazokusanywa, kuhifadhiwa, au kutumiwa na wilaya yako ya shule chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA. Shirika linaloshiriki lazima lizingatie ombi lako la kuangalia na kukagua rekodi zozote za elimu za mtoto wako bila kuchelewa kusikohitajika na kabla ya mkutano wowote kuhusu mpango wa elimu binafsi (IEP), au usikilizaji wa kesi ya mchakato wowote wa haki usio na upendeleo (ikiwa ni pamoja na mkutano wa utatuzi au kesi kuhusu nidhamu), na kwa hali yoyote lisipite siku 14 baada ya ombi lako.

Haki yako ya kuangalia na kukagua rekodi za elimu ni pamoja na:

1. Haki yako ya kupata jibu kutoka kwa shirika linaloshiriki kwa maombi yako yanayofaa ya ufafanuzi na ufasiri wa rekodi;
2. Haki yako ya kuomba kwamba shirika linaloshiriki litoe nakala za rekodi ikiwa huwezi kuangalia na kukagua rekodi isipokuwa ukipokea nakala hizo; **na**
3. Haki yako ya mwakilishi wako kuangalia na kukagua rekodi.

Shirika linaloshiriki linapaswa kuchukulia kuwa una mamlaka ya kuangalia na kukagua rekodi zinazohusiana na mtoto wako isipokuwa ikiwa limeshauriwa kuwa huna mamlaka chini ya sheria husika ya Jimbo inayosimamia mambo kama vile ulezi, kutengana na talaka.

# Ufikiaji wa Rekodi

## 34 CFR §300.614

Kila shirika linaloshiriki lazima lihifadhi rekodi ya wahusika wanaofikia rekodi za elimu zilizokusanywa, kuhifadhiwa, au kutumiwa chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA (isipokuwa ikiwa ufikiaji huo ni wa wazazi na wafanyakazi walioidhinishwa wa shirika linaloshiriki), ikiwa ni pamoja na jina la mhusika, tarehe ambayo ruhusa ya ufikiaji ilitolewa, na kusudi ambalo mhusika anaidhinishwa kutumia rekodi hizo.

## Rekodi za Zaidi ya Mtoto Mmoja

### 34 CFR §300.615

Ikiwa rekodi yoyote ya elimu inajumuisha taarifa kuhusu zaidi ya mtoto mmoja, wazazi wa watoto hao wana haki ya kuangalia na kukagua tu taarifa zinazohusiana na mtoto wao au kufahamishwa kuhusu taarifa hizo mahususi.

## Orodha ya Aina na Maeneo ya Taarifa

### 34 CFR § 300.616

Kwa ombi, kila shirika linaloshiriki lazima likupe orodha ya aina na maeneo ya rekodi za elimu zilizokusanywa, kuhifadhiwa, au kutumiwa na shirika.

## Ada

### 34 CFR § 300.617

Kila shirika linaloshiriki linaweza kutoza ada ya kutoa nakala za rekodi ambazo zinatolewa kwako chini ya Sehemu ya B ya sheria IDEA, ikiwa ada hiyo haikuzuii kutumia haki yako ya kuangalia na kukagua rekodi hizo.

Shirika linaloshiriki halipaswi kutoza ada ya kutafuta au kupata taarifa chini ya Sehemu ya B ya sheria IDEA.

## Marekebisho ya Rekodi kwa Ombi la Mzazi

### 34 CFR § 300.618

Ikiwa unaamini kuwa taarifa katika rekodi za elimu kuhusu mtoto wako zilizokusanywa, kuhifadhiwa au kutumika chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA sio sahihi, zinapotosha, au zinakiuka faragha au haki zingine za mtoto wako, unaweza kuomba shirika linaloshiriki ambalo linahifadhi taarifa hizo kubadilisha taarifa.

Shirika linaloshiriki lazima liamue ikiwa litabadilisha taarifa kulingana na ombi lako ndani ya muda unaofaa baada ya kupokea ombi lako.

Ikiwa shirika linaloshiriki litakataa kubadilisha taarifa kulingana na ombi lako, lazima likujulishe hatua yake ya kukataa na likushauri kuhusu haki yako ya kupata kikao cha usikilizaji wa kesi kama ilivyoelezwa chini ya kichwa cha ***Fursa ya Usikilizaji wa Kesi***.

## FURSA YA USIKILIZAJI WA KESI

### 34 CFR § 300.619

Shirika linaloshiriki lazima, kwa ombi lako, likupe fursa ya usikilizaji wa kesi ya kupinga taarifa iliyo katika rekodi za elimu kuhusu mtoto wako ili kuhakikisha kuwa sio sahihi, hazipotoshi au vinginevyo hazikiuki faragha au haki zingine za mtoto wako.

## TARATIBU ZA USIKILIZAJI WA KESI

### 34 CFR § 300.621

Kikao cha usikilizaji wa kesi ya kupinga taarifa iliyo katika rekodi za elimu lazima kifanyike kwa mujibu wa taratibu za vikao hivyo chini ya Sheria ya Haki za Elimu za Familia na Faragha (FERPA).

## MATOKEO YA USIKILIZAJI WA KESI

### 34 CFR § 300.620

Ikiwa, kama matokeo ya usikilizaji wa kesi, shirika linaloshiriki litaamua kuwa taarifa hizo sio sahihi, zinapotosha au vinginevyo zinakiuka faragha au haki zingine za mtoto wako, lazima libadilishe taarifa ipasavyo na kukujulisha kwa maandishi.

Ikiwa, kama matokeo ya usikilizaji wa kesi, shirika linaloshiriki litaamua kuwa taarifa hizo ni sahihi, hazipotoshi, au vinginevyo hazikiuki faragha au haki zingine za mtoto wako, lazima likujulishe haki yako ya kujumuisha maelezo kwenye taarifa au sababu zozote zinazokufanya usikubaliane na uamuzi wa shirika linaloshiriki katika rekodi ambazo linahifadhi kuhusu mtoto wako.

Maelezo hayo yanayowekwa katika rekodi za mtoto wako lazima:

1. Yahifadhiwe na shirika linaloshiriki kama sehemu ya rekodi za mtoto wako mradi tu rekodi au sehemu inayopingwa inahifadhiwa na shirika linaloshiriki; **na**
2. Ikiwa shirika linaloshiriki litafichua rekodi za mtoto wako au taarifa iliyopingwa kwa mhusika yeyote, maelezo hayo lazima pia yafichuliwe kwa mhusika huyo.

## IDHINI YA UFICHUAJI WA TAARIFA BINAFSI ZINAZOWEZA KUTAMBULISHA MTU

### 34 CFR § 300.622

Isipokuwa taarifa hizo ziko katika rekodi za elimu, na ufichuzi umeidhinishwa bila idhini ya wazazi chini ya Sheria ya Haki za Elimu za Familia na Faragha (FERPA), ni lazima utoe idhini yako kabla ya taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha mtu

kufichuliwa kwa wahusika wengine kando na maafisa wa mashirika yanayoshiriki. Isipokuwa chini ya hali zilizobainishwa hapa chini, idhini yako haihitajiki kabla ya taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha mtu kutolewa kwa maafisa wa mashirika yanayoshiriki kwa madhumuni ya kukidhi masharti ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA.

Idhini yako, au idhini ya mtoto anayestahiki ambaye amefikisha umri wa mtu mzima chini ya sheria ya Jimbo, lazima itolewe kabla ya taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha mtu kutolewa kwa maafisa wa mashirika yanayoshiriki yanayotoa au kulipia huduma za mpito.

Ikiwa mtoto wako yupo, au atajiunga na, shule ya kibinafsi ambayo haipo katika wilaya ya shule unakoishi, idhini yako lazima itolewe kabla ya taarifa zozote binafsi zinazoweza kutambulisha mtu kuhusu mtoto wako kutolewa kati ya maafisa katika wilaya ya shule ambapo shule ya kibinafsi inapatikana na maafisa katika wilaya ya shule unakoishi.

## ULINZI

### 34 CFR § 300.623

Kila shirika linaloshiriki lazima lilinde usiri wa taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha mtu katika hatua za ukusanyaji, uhifadhi, ufichuzi na uharibifu.

Afisa mmoja katika kila shirika linaloshiriki lazima achukue jukumu la kuhakikisha usiri wa taarifa yoyote binafsi inayoweza kutambulisha mtu.

Watu wote wanaokusanya au kutumia taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha mtu lazima wapokee mafunzo au maelekezo kuhusu sera na taratibu za Jimbo lako kuhusu usiri chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA na Sheria ya Haki za Elimu za Familia na Faragha (FERPA).

Kila shirika linaloshiriki lazima lihifadhi, kwa ukaguzi wa umma, orodha ya sasa ya majina na vyeo vya wafanyakazi hao ndani ya shirika ambao wanaweza kufikia taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha mtu.

## KUHARIBU TAARIFA

### 34 CFR §300.624, NH 1109.01

Wilaya yako ya shule lazima ikujulishe wakati taarifa binafsi inayoweza kutambulisha mtu iliyokusanywa, kuhifadhiwa au kutumika chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA haihitajiki tena ili kutoa huduma za elimu kwa mtoto wako.

Taarifa lazima iharibiwe kwa ombi lako. Hata hivyo, rekodi ya kudumu ya jina la mtoto wako, anwani, na nambari ya simu, alama zake, rekodi ya mahudhurio, madarasa aliyohudhuria, kiwango alichokamilisha cha gredi, na mwaka aliokamilisha zinaweza kuhifadhiwa bila kikomo cha muda.

LEA haitaharibu rekodi za elimu maalum za mwanafunzi kabla ya mwanafunzi kufikia umri wa miaka 26 bila idhini.

# TARATIBU ZA LALAMIKO LA JIMBO

## TOFAUTI KATI YA TARATIBU ZA MALALAMIKO NA USIKILIZAJI WA KESI YA MCHAKATO WA HAKI NA MALALAMIKO YA JIMBO

Kanuni za Sehemu ya B ya sheria ya IDEA zimebainisha taratibu tofauti za kuwasilisha malalamiko ya Jimbo na kwa malalamiko na usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki. Kama ilivyoelezwa hapo chini, mtu au shirika lolote linaweza kuwasilisha lalamiko la Jimbo kwa madai ya ukiukaji wa masharti yoyote ya Sehemu ya B wa wilaya ya shule, Shirika la Elimu la Jimbo, au shirika lingine lolote la umma.

Wewe au wilaya ya shule tu ndio mnaoweza kuwasilisha lalamiko la mchakato wa haki kuhusu jambo lolote linalohusiana na pendekezo au kukataa kuanzisha au kubadilisha utambuzi, tathmini, au uwekaji wa elimu wa mtoto mwenye ulemavu, au utoaji wa elimu ya bure na inayofaa ya umma (FAPE) kwa mtoto.

Ingawa wafanyakazi wa Shirika la Elimu la Jimbo kwa ujumla lazima watatue lalamiko la Jimbo ndani ya ratiba ya siku 60, isipokuwa kama ratiba ya muda itaongezwa ipasavyo, hakimu asiye na upendeleo lazima asikilize lalamiko la mchakato wa haki (ikiwa halijatatuliwa kupitia mkutano wa utatuzi au kupitia upatanisho) na atoe uamuzi wa maandishi ndani ya siku 45 baada ya kukamilika kwa kipindi cha utatuzi, kama ilivyoelezwa katika hati hii chini ya kichwa cha **Mchakato wa Utatuzi**, isipokuwa hakimu aongeze muda mahususi kwenye ratiba kwa ombi lako au ombi la wilaya ya shule. Taratibu za lalamiko la Jimbo na lalamiko la mchakato wa haki, utatuzi na usikilizaji wa kesi zimeelezewa kikamilifu hapa chini.

Shirika la Elimu la Jimbo lazima liunde fomu za mfano ili kukusaidia kuwasilisha malalamiko ya mchakato wa haki na kukusaidia wewe au wahusika wengine kuwasilisha malalamiko ya Jimbo kama ilivyoelezwa chini ya kichwa cha ***Fomu za Mfano***.

## TARATIBU ZA LALAMIKO LA JIMBO

### 34 CFR § 300.151, NH Ed 1121

#### Jumla

New Hampshire lazima iwe na taratibu zilizoandikwa kuhusiana na:

1. Kutatua lalamiko lolote, ikiwa ni pamoja na lalamiko linalowasilishwa na shirika au mtu binafsi kutoka Jimbo lingine;
2. Kuwasilisha lalamiko kwa Shirika la Elimu la Jimbo;

   Kusambaza taratibu za malalamiko ya Jimbo kwa wazazi na watu wengine wanaotaka, ikiwa ni pamoja na mafunzo ya wazazi na vituo vya habari, mashirika ya ulinzi na utetezi, vituo vya maisha ya kujitegemea, na asasi zingine zinazofaa.

### Suluhu za kunyimwa huduma zinazofaa

Katika kutatua lalamiko la Jimbo ambapo Shirika la Elimu la Jimbo limepatikana kushindwa kutoa huduma zinazofaa, Shirika la Elimu la Jimbo lazima lishughulikie:

1. Kushindwa huko kutoa huduma zinazofaa, ikiwa ni pamoja na hatua za marekebisho zinazofaa za kushughulikia mahitaji ya mtoto (kama vile huduma za ufidiaji au urejeshaji wa fedha); **na**
2. Kutoa huduma zinazofaa za usoni kwa watoto wote wenye ulemavu.

## KIKOMO CHA MUDA KWA TARATIBU ZA MALALMIKO YA JIMBO

## 34 CFR § 300.152

### Kikomo cha muda; kikomo cha muda kwa taratibu

Kila Shirika la Elimu la Jimbo lazima lijumuishe katika taratibu zake za lalamiko la Jimbo kikomo cha muda wa siku 60 baada ya lalamiko kuwasilishwa ili:

1. Kufanya uchunguzi huru kwenye eneo, ikiwa Shirika la Elimu la Jimbo litaamua kuwa uchunguzi unahitajika;
2. Kumpa mlalamikaji fursa ya kuwasilisha taarifa za ziada, ama kwa kutamka au kwa maandishi, kuhusu madai yaliyo katika lalamiko;
3. Kuipa wilaya ya shule au shirika lingine la umma fursa ya kujibu lalamiko, ikiwa ni pamoja na, kwa kiwango cha chini: (a) kwa hiari ya shirika, pendekezo la kutatua lalamiko; **na** (b) fursa kwa mzazi ambaye amewasilisha lalamiko na shirika kukubaliana kwa hiari kushiriki katika upatanisho;
4. Kukagua taarifa zote husika na kufanya uamuzi huru kuhusu ikiwa wilaya ya shule au shirika lingine la umma linakiuka masharti ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA; **na**
5. Kutoa uamuzi wa maandishi kwa mlalamikaji unaoshughulikia kila dai lililo katika lalamiko na unaojumuisha: (a) matokeo ya ukweli na hitimisho; **na** (b) sababu za uamuzi wa mwisho wa Shirika la Elimu la Jimbo.

### Uongezaji wa muda; uamuzi wa mwisho; utekelezaji

Taratibu za Shirika la Elimu la Jimbo zilizoelezwa hapo juu pia lazima:

1. Ziruhusu uongezaji wa kikomo cha muda wa siku 60 ikiwa tu: (a) kuna hali za kipekee kwa kuzingatia lalamiko maalum la Jimbo; **au** (b) wewe na wilaya ya shule au shirika lingine la umma linalohusika kwa hiari mnakubaliana kuongeza muda wa kutatua suala hilo kupitia upatanisho au njia mbadala ya utatuzi wa migogoro, ikiwa inapatikana katika Jimbo.
2. Zijumuishe taratibu za utekelezaji wenye ufanisi wa uamuzi wa mwisho wa Shirika la Elimu la Jimbo, ikiwa inahitajika, ikiwa ni pamoja na: (a) shughuli za msaada wa kiufundi; (b) mazungumzo ya pamoja; **na** (c) hatua za kurekebisha ili kupata utiifu.

### Malalamiko ya jimbo na usikilizaji wa kesi wa mchakato wa haki

Ikiwa lalamiko la maandishi la Jimbo limepokewa na linahitaji pia kushughulikiwa na usikilizaji wa kesi wa mchakato wa haki kama ilivyoelezwa chini ya kichwa cha ***Kuwasilisha Lalamiko la Mchakato wa Haki***, au lalamiko la Jimbo linajumuisha masuala kadhaa ambayo moja au zaidi ni sehemu ya usikilizaji huo wa kesi, Jimbo lazima liweke kando sehemu yoyote ya lalamiko la Jimbo inayoshughulikiwa na usikilizaji wa kesi wa mchakato wa haki hadi kesi hiyo itakapomalizika. Suala lolote katika lalamiko la Jimbo ambalo si sehemu ya usikilizaji wa kesi wa mchakato wa haki lazima litatuliwe kwa kutumia kikomo cha muda na taratibu zilizoelezwa hapo juu.

Ikiwa suala lililoibuliwa katika lalamiko la Jimbo lilifanyiwa uamuzi hapo awali katika usikilizaji kesi wa mchakato wa haki unaohusisha wahusika hao (kwa mfano, wewe na wilaya ya shule), basi uamuzi wa usikilizaji kesi wa mchakato wa haki utatumika katika suala hilo na Shirika la Elimu la Jimbo lazima limjulishe mlalamikaji kwamba uamuzi huo unatumika.

Lalamiko linalodai kuwa wilaya za shule au shirika lingine la umma limekosa kutekeleza uamuzi wa kikao cha usikilizaji kesi wa mchakato wa haki lazima yatatuliwe na Shirika la Elimu la Jimbo.

## KUWASILISHA LALAMIKO LA JIMBO

### 34 CFR § 300.153

Shirika au mtu binafsi anaweza kuwasilisha lalamiko la Jimbo lililosainiwa chini ya taratibu zilizoelezwa hapo juu.

Lalamiko la Jimbo lazima lijumuishe:

1. Taarifa kwamba wilaya ya shule au shirika lingine la umma limekiuka masharti ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA au kanuni zake za utekelezaji katika 34 CFR Sehemu ya 300;
2. Ushahidi ambao taarifa hiyo inategemea;
3. Maelezo ya mawasiliano na saini ya mhusika anayewasilisha lalamiko; na
4. Ikiwa yanadai ukiukaji kuhusu mtoto mahususi:
   (a) Jina la mtoto na anwani ya makazi ya mtoto;
   (b) Jina la shule ambayo mtoto anahudhuria;
   (c) Katika kisa cha kijana au mtoto asiye na makazi, maelezo ya mawasiliano yanayopatikana ya mtoto, na jina la shule ambayo mtoto anahudhuria;
   (d) Maelezo ya asili ya tatizo la mtoto, ikiwa ni pamoja na ushahidi unaohusiana na tatizo; **na**
   (e) Utatuzi uliopendekezwa wa tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kupatikana kwa mhusika anayewasilisha lalamiko wakati lalamiko linawasilishwa.

Lalamiko lazima lidai ukiukaji ambao ulitokea si zaidi ya mwaka mmoja kabla ya tarehe ambayo lalamiko litapokewa kama ilivyoelezwa chini ya kichwa cha ***Kupitishwa kwa Taratibu za Lalamiko la Jimbo.***

Malalamiko yanatumwa kwa barua kwa: Commissioner of Education
New Hampshire Department of Education
25 Hall Street
Concord, NH 03301

Mhusika anayewasilisha lalamiko la Jimbo lazima atume nakala ya lalamiko kwa wilaya ya shule au shirika lingine la umma linalomhudumia mtoto wakati huo huo mhusika anapowasilisha lalamiko kwa Shirika la Elimu la Jimbo.

### Ombi la Kuzingatia Upya

Mhusika yeyote kwenye lalamiko anaweza, ndani ya siku 20 baada ya kupokea uamuzi wa maandishi wa kamishna, kutoa ombi la maandishi kwa kamishna kwa ajili ya kuzingatiwa upya kwa uamuzi huo. Hatua yoyote ya kurekebisha iliyoamriwa na kamishna kwa manufaa ya mtoto mwenye ulemavu itatekelezwa na kuendelea hadi hitimisho la kuzingatia upya likifanywa na, isipokuwa kama itabadilishwa kutokana na kuzingatiwa upya au kudumishwa, wakati wa rufaa yoyote.

## FOMU ZA MFANO

### 34 CFR § 300.509

New Hampshire Department of Education imeunda fomu za mfano ili kukusaidia kuwasilisha lalamiko la mchakato wa haki na kukusaidia wewe na wahusika wengine kuwasilisha lalamiko la Jimbo. Hata hivyo, Jimbo au wilaya ya shule yako inaweza kukosa kuhitaji matumizi ya fomu hizi za mfano. Kwa hakika, unaweza kutumia fomu ya mfano au fomu nyingine inayofaa, mradi tu inajumuisha taarifa zinazohitajika ili kuwasilisha lalamiko la mchakato wa haki au lalamiko la Jimbo. Fomu za mfano zinaweza kupatikana katika www.education.nh.gov au kwa kupiga simu kwa 603-271-3196 (Malalamiko ya Jimbo) au 603-271-2299 (Mchakato wa Haki na Utatuzi Mbadala wa Migogoro).

# TARATIBU ZA LALAMIKO LA MCHAKATO WA HAKI

## KUWASILISHA LALAMIKO LA MCHAKATO WA HAKI

### 34 CFR § 300.507, NH Ed 1123

**Jumla**

Wewe au wilaya ya shule mnaweza kuwasilisha lalamiko la mchakato wa haki kuhusu jambo lolote linalohusiana na pendekezo au kukataa kuanzisha au kubadilisha utambuzi, tathmini au uwekaji wa elimu wa mtoto wako, au utoaji wa elimu ya bure na inayofaa ya umma (FAPE) kwa mtoto wako.

Lalamiko la mchakato wa haki lazima lidai ukiukaji ambao ulitokea si zaidi ya miaka miwili kabla ya wewe au wilaya ya shule kujua au kupaswa kujua kuhusu hatua inayodaiwa ambayo ni msingi wa lalamiko la mchakato wa haki.

Ratiba iliyo hapo juu haitumiki kwako ikiwa hungeweza kuwasilisha lalamiko la mchakato wa haki ndani ya ratiba kwa sababu:

1. Wilaya ya shule hasa ilitoa taarifa ya kupotosha kwamba ilikuwa imetatua masuala yaliyobainishwa katika lalamiko; **au**
2. Wilaya ya shule ilizuia usijue taarifa ambazo ilihitajika kukupa chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA.

**Taarifa kwa wazazi**

Wilaya ya shule lazima ikujulishe kuhusu huduma zozote za kisheria za bila malipo au za gharama nafuu na huduma zingine zinazofaa zinazopatikana katika eneo ikiwa utaomba taarifa hizo, au ikiwa wewe **au** wilaya ya shule itawasilisha lalamiko la mchakato wa haki.

## LALAMIKO LA MCHAKATO WA HAKI

### 34 CFR § 300.508

**Jumla**

Ili kuomba kikao cha usikilizaji wa kesi, wewe au wilaya ya shule (au wakili wako au wakili wa wilaya ya shule) lazima iwasilishe lalamiko la mchakato wa haki kwa mhusika huyo mwingine. Lalamiko hilo lazima lijumuishe maudhui yote yaliyoorodheshwa hapa chini na lazima yawekwe kwa siri.

Yeyote anayewasilisha lalamiko lazima pia atoe nakala ya lalamiko kwa Shirika la Elimu la Jimbo.

**Maudhui ya lalamiko**

Lalamiko la mchakato wa haki lazima lijumuishe:

1. Jina la mtoto;
2. Anwani ya makazi ya mtoto;
3. Jina la shule ya mtoto;
4. Ikiwa kijana au mtoto ni mtoto asiye na makazi, maelezo ya mawasiliano ya mtoto na jina la shule ya mtoto;
5. Maelezo ya asili ya tatizo la mtoto kuhusiana na hatua iliyopendekezwa au iliyokataliwa, ikiwa ni pamoja na ukweli unaohusiana na tatizo; **na**
6. Suluhu inayopendekezwa kwa tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kupatikana kwa mhusika anayelalamika (wewe au wilaya ya shule) kwa wakati huo.

**Notisi inahitajika kabla ya usikilizaji wa kesi ya lalamiko la mchakato wa haki**

Wewe au wilaya ya shule inaweza kukosa kushiriki katika usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki mpaka wewe au wilaya ya shule (au wakili wako au wakili wa wilaya ya shule) iwasilishe lalamiko la mchakato wa haki ambalo linajumuisha taarifa zilizoorodheshwa hapo juu.

**Kutosha kwa lalamiko**

Ili lalamiko la mchakato wa haki lishughulikiwe, lazima lizingatiwe kuwa la kutosha. Lalamiko la mchakato wa haki litazingatiwa kuwa la kutosha (limekidhi masharti ya maudhui yaliyo hapo juu) isipokuwa mhusika anayepokea lalamiko la mchakato wa haki (wewe au wilaya ya shule) akimjulisha hakimu na mhusika huyo mwingine kwa maandishi, ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea lalamiko, kwamba mhusika anayepokea lalamiko anaamini kuwa lalamiko la mchakato wa haki halikidhi masharti yaliyoorodheshwa hapo juu.

Ndani ya siku tano za kalenda baada ya kupokea taarifa kwamba mhusika anayepokea lalamiko (wewe au wilaya ya shule) anazingatia lalamiko la mchakato wa haki kuwa halitoshi, hakimu lazima aamue ikiwa lalamiko la mchakato wa haki linakidhi masharti yaliyoorodheshwa hapo juu, na kukujulisha wewe na wilaya ya shule kwa maandishi mara moja.

**Marekebisho ya lalamiko**

Wewe au wilaya ya shule inaweza kufanya mabadiliko kwenye lalamiko tu ikiwa:

1. Mhusika huyo mwingine anakubali mabadiliko kwa maandishi na amepewa fursa ya kutatua lalamiko la mchakato wa haki kupitia mkutano wa utatuzi, ulioelezwa chini ya kichwa cha ***Mchakato wa Utatuzi***; **au**
2. Kwa muda usiozidi siku tano kabla ya kuanza kwa usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki, hakimu atatoa ruhusa ya kufanya mabadiliko.

Ikiwa mhusika anayelalamika (wewe au wilaya ya shule) atafanya mabadiliko kwenye lalamiko la mchakato wa haki, ratiba za mkutano wa utatuzi (ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea lalamiko) na kipindi cha muda wa utatuzi (ndani ya siku 30 za kalenda baada ya kupokea lalamiko) huanza tena tarehe ambayo lalamiko lililorekebishwa linapowasilishwa.

### Jibu la shirika la elimu la eneo (LEA) au wilaya ya shule kwa lalamiko la mchakato wa haki

Ikiwa wilaya ya shule haijakutumia notisi ya maandishi, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa ***Notisi ya Awali Iliyoandikwa***, kuhusiana na suala lililomo katika lalamiko lako la mchakato wa haki, wilaya ya shule lazima, ndani ya siku 10 za kalenda baada ya kupokea lalamiko la mchakato wa haki, ikutumie jibu ambalo linajumuisha:

1. Maelezo ya kwa nini wilaya ya shule ilipendekeza au ilikataa kuchukua hatua iliyoibuliwa katika lalamiko la mchakato wa haki;
2. Maelezo ya machaguo mengine ambayo Timu ya Mpango wa Elimu Binafsi (IEP) ya mtoto wako ilizingatia na sababu kwa nini machaguo hayo yalikataliwa;
3. Maelezo ya kila utaratibu wa tathmini, ukadiriaji, rekodi, au ripoti ambayo wilaya ya shule ilitumia kama msingi wa hatua iliyopendekezwa au iliyokataliwa; **na**
4. Maelezo ya sababu zingine ambazo zinafaa kwa hatua iliyopendekezwa au kukataliwa na wilaya ya shule.

Kutoa taarifa katika vipengee vya 1-4 vilivyo hapo juu hakuzuii wilaya ya shule kudai kuwa lalamiko lako la mchakato wa haki halikutosha.

### Majibu ya mhusika huyo mwingine kwa lalamiko la mchakato wa haki

Isipokuwa kama ilivyoelezwa chini ya kichwa kidogo kilicho hapo juu, ***Jibu la Shirika la elimu la eneo (LEA) au wilaya ya shule kwa*** lalamiko la mchakato wa haki, mhusika anayepokea lalamiko la mchakato wa haki lazima, ndani ya siku 10 za kalenda baada ya kupokea lalamiko, amtumie mhusika huyo mwingine jibu ambalo linashughulikia masuala yaliyo katika lalamiko.

### Ombi Tofauti kwa ajili ya Usikilizaji wa Kesi ya Mchakato wa Haki

Hakuna chochote katika sehemu ya ulinzi wa utaratibu wa kanuni za Shirikisho chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA 2004 (34 CFR § 300.500 hadi 300.536) kinaweza kufasiriwa kukuzuia kuwasilisha lalamiko tofauti la mchakato wa haki kuhusu suala tofauti na lalamiko ulilowasilisha tayari la mchakato wa haki.

# UPATANISHO

## 34 CFR § 300.506

### Jumla

Wilaya ya shule inaweza kuweka taratibu zinazofanya upatanisho upatikane ili kukuwezesha wewe na wilaya ya shule kutatua kutokubaliana kuhusu suala lolote chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, pamoja na masuala yanayojitokeza kabla ya kuwasilisha lalamiko la mchakato wa haki. Hivyo, upatanisho unapatikana kutatua

migogoro chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, iwe umewasilisha lalamiko la mchakato wa haki au la ili kuomba usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki kama ilivyoelezwa chini ya kichwa cha ***Kuwasilisha Lalamiko la Mchakato wa Haki***.

**Masharti**

Taratibu lazima zihakikishe kuwa mchakato wa upatanisho:

1. Ni wa hiari kwa upande wako na upande wa wilaya ya shule;
2. Hautumiwi kukunyima au kuchelewesha haki yako ya kupata kikao cha usikilizaji wa mchakato wa haki, au kukunyima haki zingine zozote zinazotolewa chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA; **na**
3. Unafanywa na mpatanishi aliyehitimu na asiye na upendeleo ambaye amepata mafunzo kuhusu mbinu bora za upatanisho.

Wilaya ya shule inaweza kuweka taratibu ambazo zinawapa wazazi na shule ambazo zinachagua kutotumia mchakato wa upatanisho, fursa ya kukutana, kwa wakati na eneo linalokufaa, na mhusika asiyependelea mchakato huu:

1. Ambaye yuko chini ya mkataba na asasi mbadala ya utatuzi wa migogoro, au kituo cha mafunzo na habari kwa wazazi au kituo cha jamii cha rasilimali za wazazi katika Jimbo; **na**
2. Ambaye anaweza kuelezea faida za, na kuhimiza matumizi ya, mchakato wa upatanisho kwa wazazi.

Jimbo lazima liwe na orodha ya watu ambao ni wapatanishi waliohitimu na wanaofahamu sheria na kanuni zinazohusiana na utoaji wa elimu maalum na huduma zinazohusiana. Shirika la Elimu la Jimbo lazima lichague wapatanishi kwa nasibu, mzunguko au msingi mwingine usio na upendeleo.

Jimbo linawajibika kwa gharama za mchakato wa upatanisho, ikiwa ni pamoja na gharama za mikutano.

Kila mkutano katika mchakato wa upatanisho lazima upangwe kwa wakati unaofaa na kufanyika mahali panapofikika kwa urahisi kwako na wilaya ya shule.

Ikiwa wewe na wilaya ya shule mtatatua mgogoro kupitia mchakato wa upatanisho, pande zote mbili lazima ziingie katika makubaliano ya kisheria ambayo yanabainisha suluhu na:

1. Yanayosema kuwa majadiliano yote yaliyotokea wakati wa mchakato wa upatanisho yatabaki kuwa ya siri na hayapaswi kutumika kama ushahidi katika kikao cha usikilizaji wa kesi yoyote ya mchakato wa haki cha baadaye au mashtaka ya kiraia (kesi ya mahakama); **na**
2. Yasainiwe na wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye ana mamlaka ya kufanya mikataba ya kisheria kwa niaba ya wilaya ya shule.

Makubaliano ya upatanisho yaliyoandikwa na kusainiwa yanaweza kutekelezwa katika mahakama yoyote ya Jimbo yenye mamlaka (mahakama ambayo ina mamlaka chini ya sheria ya Jimbo kusikiliza kesi ya aina hii) au katika mahakama ya wilaya ya Marekani.

Majadiliano yaliyofanyika wakati wa mchakato wa upatanisho lazima yawe ya siri. Hayawezi kutumika kama ushahidi katika usikilizaji wa kesi yoyote ya baadaye ya mchakato wa haki au mashtaka ya kiraia katika mahakama yoyote ya Shirikisho au mahakama ya Jimbo inayopokea msaada chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA.

**Mpatanishi asiye na upendeleo**

Mpatanishi:

1. Hapaswi kuwa mfanyakazi wa Shirika la Elimu la Jimbo au wilaya ya shule ambayo inahusika katika elimu au huduma za mtoto wako; **na**
2. Hapaswi kuwa na maslahi ya kibinafsi au ya kitaalamu ambayo yanakwaza uwezo wa mpatanishi wa kutokuwa na upendeleo.

Mtu ambaye vinginevyo anastahiki kama mpatanishi sio mfanyakazi wa wilaya ya shule au shirika la Jimbo kwa sababu tu analipwa na shirika au wilaya ya shule kuhudumu kama mpatanishi.

# UTARATIBU WA UTATUZI

## 34 CFR § 300.510

### Mkutano wa Utatuzi

Ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea notisi ya lalamiko lako la mchakato wa haki, na kabla ya kuanza kwa vikao vya usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki, wilaya ya shule lazima ikutane na wewe na washirika husika au washirika wa Timu ya Mpango wa Elimu Binafsi (IEP) ambao wana ujuzi maalum wa ukweli uliotambuliwa katika lalamiko lako la mchakato wa haki. Mkutano huo:

1. Lazima ujumuishe mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye ana mamlaka ya kufanya maamuzi kwa niaba ya wilaya ya shule; **na**
2. Haupaswi kujumuisha wakili wa wilaya ya shule isipokuwa wewe mwenyewe una wakili wako.

Mzazi pamoja na wilaya ya shule huamua washiriki husika wa Timu ya IEP watakaohudhuria mkutano huo.

Madhumuni ya mkutano ni wewe kujadili lalamiko lako la mchakato wa haki, na ukweli unaounda msingi wa lalamiko hilo, ili wilaya ya shule iwe na fursa ya kutatua mgogoro.

Mkutano wa utatuzi sio lazima ufanyike ikiwa:

1. Wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kwa maandishi kutofanya mkutano; **au**
2. Wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kutumia mchakato wa upatanisho, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa cha ***Upatanisho***.

### Kipindi cha utatuzi

Ikiwa wilaya ya shule haijatatua lalamiko la mchakato wa haki kwa njia inayokuridhisha ndani ya siku 30 za kalenda baada ya kupokea lalamiko la mchakato wa haki (wakati wa kipindi cha mchakato wa utatuzi), kikao cha usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki kinaweza kuandaliwa.

Ratiba ya siku 45 za kalenda ya kutoa uamuzi wa mwisho wa usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa, ***Maamuzi ya Usikilizaji wa Kesi***, huanza wakati wa kumalizika kwa kipindi cha utatuzi cha siku 30 za kalenda,

lakini kuna hali maalum zinazotumika kwa marekebisho yaliyofanywa kwa kipindi cha utatuzi cha siku 30 za kalenda, kama ilivyoelezwa hapa chini.

Isipokuwa wakati ambapo wewe na wilaya ya shule mmekubaliana kuondoa mchakato wa utatuzi au kutumia upatanisho, kukosa kwako kushiriki katika mkutano wa utatuzi kutacheleweshа ratiba za mchakato wa utatuzi na usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki hadi mkutano ufanyike.

Ikiwa baada ya kufanya juhudi za kutosha na kuweka kumbukumbu ya juhudi hizo, wilaya ya shule haiwezi kupata ushiriki wako katika mkutano wa utatuzi, wilaya ya shule inaweza, mwishoni mwa kipindi cha utatuzi cha siku 30, kuomba kwamba hakimu atupilie mbali lalamiko lako la mchakato wa haki. Hati za juhudi hizo lazima zijumuishe rekodi ya majaribio ya wilaya ya shule ya kupanga muda na mahali panapokubaliwa, kama vile:

1. Rekodi za kina za simu zilizopigwa au kujaribiwa na matokeo ya simu hizo;
2. Nakala za barua za mawasiliano zilizotumwa kwako na majibu yoyote yaliyopokewa; na
3. Rekodi za kina za ziara zilizofanywa nyumbani kwako au mahali pa kazi na matokeo ya ziara hizo.

Ikiwa wilaya ya shule itakosa kufanya mkutano wa utatuzi ndani ya siku 15 baada ya kupokea notisi ya lalamiko lako la mchakato wa haki **au** ikikosa kushiriki katika mkutano wa utatuzi, unaweza kuomba hakimu aanze ratiba ya siku ya 45 za kalenda ya usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki.

### Marekebisho ya kipindi cha utatuzi cha siku 30 za kalen

Ikiwa wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kwa maandishi kuondoa mkutano wa utatuzi, basi ratiba ya siku ya 45 za kalenda ya siku ya usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki huanza siku inayofuata.

Baada ya kuanza kwa mchakato wa upatanisho au mkutano wa utatuzi na kabla ya mwisho wa kipindi cha utatuzi cha siku 30 za kalenda, ikiwa wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kwa maandishi kwamba hakuna makubaliano yanayowezekana, basi ratiba ya siku 45 za kalenda ya usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki huanza siku inayofuata.

Ikiwa wewe na wilaya ya shule mtakubali kutumia mchakato wa upatanisho lakini bado hamjafikia makubaliano, mwishoni mwa kipindi cha utatuzi cha siku 30 za kalenda, mchakato wa upatanisho unaweza kuendelea hadi makubaliano yatakapofikiwa ikiwa pande zote mbili zinakubaliana kuendelea kwa maandishi. Hata hivyo, ikiwa wewe au wilaya ya shule itajiondoa kutoka kwa mchakato wa upatanisho wakati wa kipindi hiki cha mwendeleo, basi ratiba ya siku ya 45 za kalenda ya usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki huanza siku inayofuata.

### Makubaliano ya maafikiano ya maandishi

Ikiwa suluhu la mgogoro limefikiwa katika mkutano wa utatuzi, wewe na wilaya ya shule lazima muingie katika makubaliano ya kisheria ambayo:

1. Yamesainiwa na wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye ana mamlaka ya kufanya makubaliano ya kisheria kwa niaba ya wilaya ya shule; **na**

2. Yanaweza kutekelezeka katika mahakama yoyote ya Jimbo yenye mamlaka husika (mahakama ya Jimbo ambayo ina mamlaka ya kusikiliza aina hii ya kesi) au katika mahakama ya wilaya ya Marekani au kwa Shirika la Elimu la Jimbo, ikiwa Jimbo lako lina mbinu nyingine au taratibu zinazoruhusu wahusika kutafuta utekelezaji wa makubaliano ya utatuzi.

**Kipindi cha ukaguzi wa makubaliano**

Kama wewe na wilaya ya shule mtaingia katika makubaliano kama matokeo ya mkutano wa utatuzi, mhusika yeyote (wewe au wilaya ya shule) anaweza kubatilisha makubaliano hayo ndani ya siku 3 za kazi baada ya wewe na wilaya ya shule kusaini makubaliano.

# USIKILIZAJI WA KESI ZA MALALAMIKO YA MCHAKATO WA HAKI

## USIKILIZAJI WA KESI USIO NA UPENDELEO WA MCHAKATO WA HAKI

## 34 CFR § 300.511, NH Ed 1123

### Jumla

Wakati wowote lalamiko la mchakato wa haki linapowasilishwa, wewe au wilaya ya shule inayohusika katika mgogoro lazima ipate fursa ya kupata kikao cha usikilizaji wa kesi usio na upendeleo wa mchakato wa haki, kama ilivyoelezwa katika sehemu za ***Lalamiko la Mchakato wa Haki*** na ***Mchakato wa Utatuzi***.

### Hakimu asiye na upendeleo

Kwa kiwango cha chini zaidi, hakimu:

1. Hapaswi kuwa mfanyakazi wa Shirika la Elimu la Jimbo au wilaya ya shule ambayo inahusika katika elimu au huduma za mtoto. Hata hivyo, mtu sio mfanyakazi wa shirika kwa sababu tu analipwa na shirika kuhudumu kama hakimu;
2. Hapaswi kuwa na maslahi ya kibinafsi au ya kitaaluma ambayo yanakwaza uwezo wa hakimu wa kutokuwa na upendeleo.
3. Lazima awe na ujuzi na kuelewa masharti ya sheria ya IDEA, kanuni za Shirikisho na Jimbo zinazohusiana na IDEA, na fasiri za kisheria za IDEA na mahakama za Shirikisho na Jimbo; **na**
4. Lazima awe na ujuzi na uwezo wa kuandaa vikao vya usikilizaji, na kufanya na kuandika maamuzi, kulingana na mbinu sahihi ya kisheria.

Kila wilaya ya shule ambayo imeweka michakato ya utatuzi wa migogoro nje ya michakato ya jimbo lazima iwe na orodha ya watu wanaohudumu kama mahakimu ambayo inajumuisha taarifa ya sifa za kila hakimu.

### Suala la usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki

Mhusika (wewe au wilaya ya shule) ambaye anaomba usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki haruhusiwi kuongeza masuala katika usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki ambayo hayakuangaziwa katika lalamiko la mchakato wa haki, isipokuwa kama mhusika huyo mwingine anakubali.

### Ratiba ya kuomba kikao cha usikilizaji wa kesi

Wewe au wilaya ya shule lazima iombe kikao cha usikilizaji wa kesi usio na upendeleo kuhusiana na lalamiko la mchakato wa haki ndani ya miaka miwili baada ya tarehe ambayo wewe au wilaya ya shule ilifahamu au ilipaswa kufahamu kuhusu suala lililoangaziwa katika lalamiko.

### Hali maalum kuhusu ratiba ya wakati

Ratiba iliyo hapo juu haitumiki kwako ikiwa hukuweza kuwasilisha lalamiko la mchakato wa haki kwa sababu:

1. Wilaya ya shule hasa ilitoa taarifa ya kupotosha kwamba ilikuwa imetatua tatizo au suala ambalo unaibua katika lalamiko lako; **au**
2. Wilaya ya shule ilikuzuia kujua taarifa ambazo ilihitajika kukupa chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA.

# HAKI ZA KUPATA USIKILIZAJI WA KESI

## 34 CFR § 300.512

### Jumla

Una haki ya kujiwakilisha mwenyewe katika usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki. Aidha, mhusika yeyote katika usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki (ikiwa ni pamoja na usikilizaji wa kesi inayohusiana na taratibu za nidhamu) ana haki ya:

1. Kuandamana na kushauriwa na wakili na/au watu wenye ujuzi au mafunzo maalum kuhusu matatizo ya watoto wenye ulemavu;
2. Kuwakilishwa katika usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki na mtu ambaye ni wakili au asiye wakili;
3. Kuwasilisha ushahidi na kupinga, kuhoji, na kuhitaji mahudhurio ya mashahidi;
4. Kuzuia kuletwa kwa ushahidi wowote katika kesi ambao haujafichuliwa kwa mhusika huyo angalau siku tano za kazi kabla ya usikilizaji wa kesi;
5. Kupata rekodi ya maandishi, au, kwa chaguo lako, rekodi ya kielektroniki, ya neno kwa neno ya usikilizaji wa kesi; **na**
6. Kupata hitimisho la ukweli na maamuzi kwa maandishi, au, kwa chaguo lako, kielektroniki.

### Ufichuaji wa ziada wa taarifa

Angalau siku tano za kazi kabla ya usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki, wewe na wilaya ya shule lazima mwambiane tathmini zote zilizokamilishwa kufikia tarehe hiyo na mapendekezo kulingana na tathmini hizo ambayo wewe au wilaya ya shule mnakusudia kutumia wakati wa usikilizaji wa kesi.

Hakimu anaweza kumzuia mhusika yeyote anayekosa kuzingatia masharti haya kuleta tathmini au mapendekezo husika wakati wa usikilizaji wa kesi bila idhini ya mhusika huyo mwingine.

### Haki za wazazi wakati wa usikilizaji wa kesi

Lazima upewe haki ya:

1. Mtoto wako kuwepo wakati wa usikilizaji wa kesi;
2. Kuruhusu umma uhudhurie kikao; **na**
3. Kupewa bila malipo rekodi ya usikilizaji wa kesi, hitimisho la ukweli na maamuzi yaliyotolewa.

# MAAMUZI YA USIKILIZAJI WA KESI

## 34 CFR § 300.513

### Uamuzi wa hakimu

Uamuzi wa hakimu kuhusu ikiwa mtoto wako alipokea elimu ya bure na inayofaa ya umma (FAPE) lazima uwe na msingi wa ushahidi na hoja zinazohusiana moja kwa moja na FAPE.

Katika masuala yanayodai ukiukaji wa utaratibu (kama vile "Timu ya IEP ambayo haijakamilika"), hakimu anaweza kuamua kuwa mtoto wako hakupokea FAPE ikiwa tu ukiukaji wa utaratibu:

1. Uliingilia haki ya mtoto wako ya kupata elimu ya bure na inayofaa ya umma (FAPE);
2. Uliingilia pakubwa fursa yako ya kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi kuhusu utoaji wa elimu ya bure na inayofaa ya umma (FAPE) kwa mtoto wako; **au**
3. Ulimfanya mtoto wako akose manufaa ya elimu.

Hakuna masharti yaliyoelezwa hapo juu yanayoweza kufasiriwa kuzuia hakimu kuiamuru wilaya ya shule kutii masharti yaliyo katika sehemu ya ulinzi wa utaratibu wa kanuni za Shirikisho chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA (34 CFR § 300.500 hadi 300.536).

### Ombi tofauti la usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki

Hakuna chochote katika sehemu ya ulinzi wa utaratibu wa kanuni za Shirikisho chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA (34 CFR § 300.500 hadi 300.536) kinaweza kufasiriwa kukuzuia kuwasilisha lalamiko tofauti la mchakato wa haki kuhusu suala ambalo ni tofauti na lalamiko ulilowasilisha tayari la mchakato wa haki.

### Matokeo na uamuzi unaotolewa kwa jopo la ushauri na umma kwa ujumla

Shirika la Elimu la Jimbo, baada ya kufuta taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha mtu, lazima:

1. Litoe matokeo na maamuzi yaliyofanywa katika usikilizaji wa kesi ya mchakato haki au rufaa kwa jopo la ushauri la elimu maalum la Jimbo; **na**
2. Litoe matokeo na maamuzi hayo kwa umma.

# RUFAA

## UAMUZI WA MWISHO; RUFAA; UKAGUZI USIO NA UPENDELEO

## 34 CFR § 300.514

### Uamuzi wa mwisho wa usikilizaji wa kesi

Uamuzi unaofanywa katika usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki (ikiwa ni pamoja na usikilizaji wa kesi inayohusiana na taratibu za kinidhamu) ni wa mwisho, isipokuwa mhusika yeyote wa usikilizaji wa kesi (wewe au wilaya ya shule) anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo kwa kufungua kesi ya kiraia, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa cha ***Kesi za Kiraia, Ikiwa ni Pamoja na Kipindi cha Muda cha Kuwasilisha Kesi Hizo***.

### Matokeo na uamuzi unaotolewa kwa jopo la ushauri na umma kwa ujumla

Shirika la Elimu la Jimbo, baada ya kufuta taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha mtu, lazima:

1. Litoe matokeo na maamuzi ya rufaa kwa jopo la ushauri la elimu maalum la Jimbo; **na**
2. Litoe matokeo na maamuzi hayo kwa umma.

## RATIBA NA UFAAFU WA UKAGUZI WA USIKILIZAJI WA KESI

### 34 CFR § 300.515

Shirika la Elimu la Jimbo lazima lihakikishe ndani ya siku 45 za kalenda baada ya kumalizika kwa kipindi cha siku 30 za kalenda cha mikutano ya utatuzi **au**, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa kidogo cha ***Marekebisho ya kipindi cha utatuzi cha siku 30 za kalenda,*** bila kuzidi siku 45 za kalenda baada ya kumalizika kwa kipindi cha muda kilichorekebishwa:

1. Uamuzi wa mwisho umefikiwa katika kikao hicho cha usikilizaji wa kesi; **na**
2. Nakala ya uamuzi huo imetumwa kwa kila mhusika.

Hakimu anaweza kuongeza muda mahususi zaidi kwa kipindi cha siku 45 za kalenda kilichoelezwa hapo juu kwa ombi la mhusika yeyote (wewe au wilaya ya shule).

Kila kikao cha usikilizaji wa kesi lazima kifanyike kwa wakati na mahali ambapo ni rahisi kwako na mtoto wako kufika.

## KESI ZA KIRAIA, IKIWA NI PAMOJA NA KIPINDI CHA MUDA WA KUWASILISHA KESI HIZO

### 34 CFR § 300.516

**Jumla**

Mhusika yeyote (wewe au wilaya ya shule) ambaye hakubaliani na matokeo na uamuzi katika usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki (ikiwa ni pamoja na kesi kuhusiana na taratibu za kinidhamu) ana haki ya kuanzisha kesi ya kiraia kuhusiana na suala lililowasilishwa katika usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki. Kesi hiyo inaweza kuwasilishwa katika mahakama ya Jimbo yenye mamlaka husika (mahakama ya Jimbo ambayo ina mamlaka ya kusikiliza kesi ya aina hii) au katika mahakama ya wilaya ya Marekani bila kujali kiasi cha mgogoro.

**Kikomo cha muda**

Mhusika (wewe au wilaya ya shule) anayeanzisha kesi hiyo atakuwa na siku 90 kutoka tarehe ya uamuzi wa hakimu kuwasilisha kesi ya kiraia.

**Taratibu za ziada**

Katika kesi yoyote ya kiraia, mahakama:

1. Hupokea rekodi za kesi za utawala;
2. Husikiliza ushahidi wa ziada kwa ombi lako au kwa ombi la wilaya ya shule; **na**
3. Hutoa uamuzi wake kulingana na uzito wa ushahidi na kutoa suluhu ambalo mahakama huamua kuwa ni sahihi.

Katika hali zinazofaa, suluhu la mahakama linaweza kujumuisha marejesho ya ada ya masomo ya shule ya kibinafsi na huduma za elimu za ufidiaji.

**Mamlaka ya mahakama za wilaya**

Mahakama za wilaya za Marekani zina mamlaka ya kutoa uamuzi kuhusu kesi zilizowasilishwa chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA bila kujali kiasi cha mgogoro.

**Kanuni ya muundo**

Hakuna chochote katika Sehemu ya B ya sheria ya IDEA kinachoweka kikomo au kuzuia haki, taratibu, na suluhu zinazopatikana chini ya katiba ya Marekani, Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya 1990, Kichwa cha V cha Sheria ya Uwezeshaji wa Kuisha Maisha ya Kawaida ya 1973 (Sehemu ya 504), au sheria zingine za Shirikisho zinazolinda haki za watoto wenye ulemavu, isipokuwa kwamba kabla ya kuwasilisha kesi ya kiraia chini ya sheria hizi kutafuta suluhu ambalo pia linapatikana chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, taratibu za mchakato wa haki zilizoelezwa hapo juu lazima zitumiwe kikamilifu kwa kiwango sawa na inavyohitajika ikiwa mhusika aliwasilisha kesi hiyo chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA. Hii inamaanisha kuwa unaweza kuwa na suluhu zinazopatikana chini ya sheria zingine ambazo zinaingiliana na zile zinazopatikana chini ya sheria ya IDEA, lakini kwa ujumla, ili kupata suluhu chini ya sheria hizo zingine, lazima kwanza utumie suluhu zinazopatikana za kiutawala chini ya sheria ya IDEA (yaani, lalamiko la mchakato wa haki; mchakato wa utatuzi, ikiwa ni pamoja na mkutano wa utatuzi; na taratibu za usikilizaji wa kesi usio na upendeleo wa mchakato wa haki) kabla ya kwenda moja kwa moja mahakamani.

# Uwekaji wa Mtoto Wakati Lalamiko na Usikilizaji wa Kesi ya Mchakato wa Haki Unasubiriwa

## 34 CFR § 300.518

Isipokuwa kama ilivyoelezwa hapa chini, chini ya kichwa cha ***TARATIBU WAKATI WA KUWAADHIBU WATOTO WENYE ULEMAVU,*** mara tu lalamiko la mchakato wa haki linapotumwa kwa mhusika huyo mwingine, wakati wa kipindi cha mchakato wa utatuzi, na wakati wa kusubiri uamuzi wa usikilizaji wowote wa kesi usio na upendeleo wa mchakato wa haki au kesi ya mahakamani, isipokuwa wewe na Jimbo au wilaya ya shule mtakubaliana vinginevyo, mtoto wako lazima abaki katika uwekaji wake wa sasa wa elimu.

Ikiwa lalamiko la mchakato wa haki linahusisha ombi la kuandikishwa katika shule ya umma kwa mara ya kwanza, mtoto wako, kwa idhini yako, lazima awekwe katika mpango wa kawaida wa shule ya umma hadi kesi zote hizo zikikamilika.

Ikiwa lalamiko la mchakato wa haki linahusisha ombi la huduma za kwanza chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA kwa mtoto ambaye anabadilisha kutoka kuhudumiwa chini ya Sehemu ya C ya sheria ya IDEA hadi Sehemu ya B ya sheria ya IDEA na ambaye hastahiki tena huduma za Sehemu ya C kwa sababu mtoto amefikisha umri wa miaka mitatu, wilaya ya shule haihitajiki kutoa huduma za Sehemu ya C ambazo mtoto amekuwa akipokea. Ikiwa mtoto atapatikana anastahiki chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA na unakubali mtoto wako kupata elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza, basi, ikisubiri matokeo ya kesi, wilaya ya shule lazima itoe elimu hiyo maalum na huduma zinazohusiana ambazo hazipingwi (zile ambazo wewe na wilaya ya shule mnakubaliana).

Ikiwa hakimu katika usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki uliofanywa na Shirika la Elimu la Jimbo anakubaliana na wewe kwamba mabadiliko ya uwekaji ni sahihi, uwekaji huo lazima uchukuliwe kama uwekaji wa sasa wa mtoto wako ambapo mtoto wako atabaki wakati akisubiri uamuzi wa usikilizaji kesi usio na upendeleo wa mchakato wa haki au kesi ya mahakama.

# ADA ZA WAKILI

## 34 CFR §300.517, NH Ed 1123.22, RSA 186-c: 16-b, V

**Jumla**

Katika kesi au mashtaka yoyote yaliyofunguliwa chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, mahakama, kwa hiari yake, inaweza kufanya uamuzi wa kufidiwa ada zinazofaa za wakili kama sehemu ya gharama zako, ikiwa utashinda.

Katika kesi au mashtaka yoyote yaliyofunguliwa chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, mahakama, kwa hiari yake, inaweza kutoa uamuzi wa kufidiwa ada zinazofaa za wakili kama sehemu ya gharama kwa Shirika la Elimu la Jimbo au wilaya ya shule, zinazofaa kulipwa na wakili wako, ikiwa wakili: (a) aliwasilisha lalamiko au kesi ya mahakama ambayo mahakama inaona kuwa haina maana, sio ya busara au haina msingi; **au** (b) aliendelea kutoa madai baada ya madai hayo kuchukuliwa kuwa yasiyo na maana, yasiyo ya busara, au yasiyo na msingi; **au**

Katika kesi au mashtaka yoyote yanayowasilishwa chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, mahakama, kwa hiari yake, inaweza kutoa uamuzi wa kufidiwa ada zinazofaa za wakili kama sehemu ya gharama kwa Shirika la Elimu la Jimbo au wilaya ya shule, ambazo zinapaswa kulipwa na wewe au wakili wako, ikiwa ombi lako la usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki au baadaye kesi ya mahakama iliwasilishwa kwa madhumuni yoyote yasiyofaa, kama vile kusumbua, kusababisha ucheleweshaji usiohitajika, au kuongeza gharama ya kesi au mashtaka (usikilizaji wa kesi).

Mzazi ambaye ni mhusika aliyeshinda katika ama kesi ya mchakato wa haki au rufaa ya mahakama ya uamuzi wa Hakimu, anaweza kuwa na haki ya kurejeshewa ada zinazofaa za wakili. Kwa mujibu wa RSA 186-C: 16-b, V, mzazi lazima awasilishe ombi la kurejeshewa ada za wakili katika mahakama ya jimbo au shirikisho ndani ya siku 120 baada ya kupokea uamuzi wa Hakimu.

**Kufidiwa ada**

Mahakama hufanya uamuzi wa kufidiwa ada zinazofaa za wakili ifuatavyo:

1. Ada lazima zizingatie viwango vinavyotumika katika jamii ambayo kesi au mashtaka yaliibuka kwa aina na ubora wa huduma zilizotolewa. Hakuna bonasi au vizidishaji vinapaswa kutumika katika kuhesabu ada iliyofidiwa.
2. Ada za wakili hazipaswi kufidiwa na gharama zinazohusiana hazipaswi kurejeshwa kwa kesi au mashtaka yoyote chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA kwa huduma zilizotolewa baada yako kupewa ofa ya maafikiano ikiwa:
    a. Ofa hiyo itatolewa ndani ya muda uliowekwa na Kanuni ya 68 ya Kanuni za Shirikisho za Utaratibu wa Kiraia au, ikiwa kuna usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki au ukaguzi wa kiwango cha Jimbo, wakati wowote zaidi ya siku 10 za kalenda kabla ya mashtaka kuanza;
    b. Ofa hiyo itakosa kukubaliwa ndani ya siku 10; **na**
    c. Mahakama au hakimu wa kesi za utawala atagundua kwamba suluhu ambalo hatimaye ulipata sio zuri zaidi ikilinganishwa na ofa ya maafikiano.

Licha ya vikwazo hivi, fidia ya ada ya wakili na gharama zinazohusiana inaweza kulipwa kwako ikiwa utashinda, na ulikuwa na haki inayotosha kukataa ofa ya maafikiano.

3. Ada haziwezi kufidiwa kuhusiana na mkutano wowote wa Timu ya Mpango wa Elimu Binafsi (IEP) isipokuwa ikiwa mkutano utafanyika kama matokeo ya mashtaka ya usimamizi au kesi ya mahakama.

   Mkutano wa utatuzi, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa cha ***Mchakato wa Utatuzi***, hauchukuliwi kuwa mkutano uliofanywa kama matokeo ya usikilizaji wa kesi za kiutawala au kesi ya mahakama, na pia hauzingatiwi kuwa usikilizaji wa kesi ya kiutawala au kesi ya mahakama kwa madhumuni ya kutolewa kwa ada hizi za wakili.

Mahakama hupunguza, kama inavyofaa, kiasi cha ada za wakili kinachofidiwa chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, ikiwa mahakama itagundua kuwa:

1. Wewe, au wakili wako, wakati wa kesi au mashtaka, bila sababu alicheleweshа utatuzi wa mwisho wa mgogoro;
2. Kiasi cha ada ya wakili vinginevyo kilichoidhinishwa kufidiwa kinazidi isivyostahili kiwango cha saa kinachotumika katika jamii kwa huduma sawa za mawakili wenye ujuzi, sifa, na uzoefu sawa;
3. Muda uliotumika na huduma za kisheria zilizotolewa zilikuwa nyingi mno kwa kuzingatia asili ya kesi au mashtaka; **au**
4. Wakili anayekuwakilisha hakuipa wilaya ya shule taarifa sahihi katika notisi ya ombi la usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki kama ilivyoelezwa chini ya kichwa cha ***Lalamiko la Mchakato wa Haki***.

Hata hivyo, mahakama huenda isipunguze ada ikiwa mahakama itabaini kwamba Jimbo au wilaya ya shule bila sababu ilicheleweshа utatuzi wa mwisho wa kesi au mashtaka au kulikuwa na ukiukaji chini ya masharti ya ulinzi wa utaratibu wa Sehemu ya B ya sheria ya IDEA.

# TARATIBU WAKATI WA KUWAADHIBU WATOTO WENYE ULEMAVU

## MAMLAKA YA WAFANYAKAZI WA SHULE

## 34 CFR § 300.530

### Uamuzi kulingana na kila kisa

Wafanyakazi wa shule wanaweza kuzingatia hali yoyote ya kipekee kwa msingi wa kisa maalum wakati wa kuamua ikiwa mabadiliko ya uwekaji, yanayofanywa kulingana na mahitaji yafuatayo yanayohusiana na nidhamu, yanafaa kwa mtoto mwenye ulemavu ambaye anakiuka kanuni ya shule ya maadili mema ya mwanafunzi.

### Jumla

Kwa kiwango ambacho pia wanachukua hatua hiyo kwa watoto wasio na ulemavu, wafanyakazi wa shule wanaweza, kwa muda usiozidi **siku 10 za shule** za mfululizo, kumwondoa mtoto mwenye ulemavu ambaye anakiuka kanuni ya maadili mema ya mwanafunzi kutoka kwa uwekaji wake wa sasa hadi mazingira mbadala yanayofaa ya elimu ya muda, mazingira mengine, au kusimamishwa kuhudhuria shule. Wafanyakazi wa shule wanaweza pia kulazimisha kuondolewa kwa ziada kwa mtoto kwa muda usiozidi **siku 10 za shule** za mfululizo katika mwaka huo huo wa shule kwa matukio tofauti ya utovu wa nidhamu, mradi hatua hizo za kuondolewa hazijumuishi mabadiliko ya uwekaji (tazama kichwa cha ***Mabadiliko ya Uwekaji Kwa Sababu ya Uondoaji wa Kinidhamu*** kwa ufafanuzi).

Mara tu mtoto mwenye ulemavu anapoondolewa kutoka kwa uwekaji wake wa sasa kwa jumla ya **siku 10 za shule** katika mwaka huo huo wa shule, wilaya ya shule lazima, wakati wa siku zozote zinazofuata za kuondolewa katika mwaka huo wa shule, itoe huduma kwa kiwango kinachohitajika chini ya kichwa kidogo cha ***Huduma***.

### Mamlaka ya ziada

Ikiwa tabia iliyokiuka kanuni ya maadili mema ya mwanafunzi haikuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto (tazama kichwa kidogo cha ***Ubainishaji wa Udhihirisho***) na nidhamu ya mabadiliko ya uwekaji inazidi **siku 10 za shule** za mfululizo, wafanyakazi wa shule wanaweza kutumia taratibu za nidhamu kwa mtoto huyo mwenye ulemavu kwa njia sawa na kwa muda sawa na watoto wasio na ulemavu, isipokuwa kwamba shule lazima itoe huduma kwa mtoto huyo kama ilivyoelezwa hapa chini, chini ya ***Huduma***. Timu ya IEP ya mtoto hubaini mazingira mbadala wa elimu ya muda kwa huduma hizo.

### Huduma

Wilaya ya shule haitoi huduma kwa mtoto mwenye ulemavu au mtoto asiye na ulemavu ambaye ameondolewa kwenye uwekaji wake wa sasa kwa **siku 10 za shule au chache** katika mwaka huo wa shule.

Mtoto mwenye ulemavu ambaye ameondolewa kutoka kwa uwekaji wa sasa wa mtoto kwa **zaidi ya siku 10 za shule** na tabia sio udhihirisho wa ulemavu wa mtoto (tazama kichwa kidogo, ***Ubainishaji wa Udhihirisho***) au ambaye ameondolewa chini ya hali maalum (tazama kichwa kidogo cha ***Hali maalum***) lazima:

1. Aendelee kupokea huduma za elimu (apate elimu ya bure na inayofaa ya umma), ili kumwezesha mtoto huyo kuendelea kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, ingawa katika mazingira mengine (ambayo yanaweza kuwa mazingira mbadala ya elimu ya muda), na kuendelea kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto; **na**
2. Apokee, kama inavyofaa, tathmini ya tabia ya utendaji, na huduma za usaidizi wa tabia na marekebisho, zinazolenga kushughulikia ukiukaji wa tabia ili isitokee tena.

Baada ya mtoto mwenye ulemavu kuondolewa kutoka kwa uwekaji wake wa sasa kwa **siku 10 za shule** katika mwaka huo huo wa shule, na **ikiwa** kuondolewa kwa sasa ni kwa **siku 10 za shule** za mfululizo au chache **na** ikiwa kuondolewa huko sio mabadiliko ya uwekaji (tazama ufafanuzi hapa chini), **basi** wafanyakazi wa shule, kwa kushauriana na angalau mmoja wa walimu wa mtoto, huamua kiwango cha huduma zinazohitajika ili kumwezesha mtoto kuendelea kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, ingawa katika mazingira mengine, na kuendelea kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto.

Ikiwa kuondolewa ni mabadiliko ya uwekaji (tazama kichwa, ***Mabadiliko ya Uwekaji kwa Sababu ya Uondoaji wa Kinidhamu***), Timu ya IEP ya mtoto huamua huduma zinazofaa ili kumwezesha mtoto kuendelea kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, ingawa katika mazingira mengine (ambayo yanaweza kuwa mazingira mbadala ya elimu ya muda), na kuendelea kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto.

### Ubainishaji wa udhihirisho

Ndani ya **siku 10 za shule** baada ya uamuzi wowote wa kubadilisha uwekaji wa mtoto mwenye ulemavu kwa sababu ya ukiukaji wa kanuni ya maadili mema ya mwanafunzi (isipokuwa kwa uondoaji ambao ni wa **siku 10 za shule** ambazo ni mfululizo au chache na sio mabadiliko ya uwekaji), wilaya ya shule, wewe, na washirika wengine husika wa Timu ya IEP (kama ilivyoamuliwa nawe na wilaya ya shule) lazima mkague taarifa zote husika katika faili ya mwanafunzi, ikiwa ni pamoja na

IEP ya mtoto, maoni yoyote ya mwalimu, na taarifa yoyote husika iliyotolewa nawe ili kuamua:

1. Ikiwa mwenendo uliohusika ulisababishwa na, au ulikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na mkubwa na, ulemavu wa mtoto; **au**
2. Ikiwa mwenendo uliohusika ulikuwa matokeo ya moja kwa moja ya wilaya ya shule kukosa kutekeleza IEP ya mtoto.

Ikiwa wilaya ya shule, wewe, na washirika wengine husika wa Timu ya IEP ya mtoto mtaamua kuwa mojawapo ya hali hizo ilitimizwa, mwenendo lazima uamuliwe kuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto.

Ikiwa wilaya ya shule, wewe, na washirika wengine husika wa Timu ya IEP ya mtoto mtaamua kuwa mwenendo uliohusika ulikuwa matokeo ya moja kwa moja ya wilaya ya shule kukosa kutekeleza IEP, wilaya ya shule lazima ichukue hatua za haraka ili kurekebisha upungufu huo.

### Ubainishaji kuwa tabia hiyo ilikuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto

Ikiwa wilaya ya shule, wewe, na washirika wengine husika wa Timu ya IEP mtaamua kuwa mwenendo huo ulikuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto, Timu ya IEP lazima ama:

1. Ifanye tathmini ya tabia ya utendaji, isipokuwa ikiwa wilaya ya shule ilikuwa imefanya tathmini ya tabia ya utendaji kabla ya tabia ambayo ilisababisha mabadiliko ya uwekaji kutokea, na itekeleze mpango wa usaidizi wa tabia kwa mtoto; **au**
2. Ikiwa mpango wa usaidizi wa tabia tayari umeundwa, ikague mpango wa usaidizi wa tabia, na iubadilishe, kama inavyohitajika, ili kushughulikia tabia hiyo.

Isipokuwa kama ilivyoelezwa hapa chini, chini ya kichwa kidogo cha ***Hali maalum***, wilaya ya shule lazima irudishe mtoto wako kwa uwekaji ambao mtoto wako aliondolewa, isipokuwa wewe na wilaya mnakubali mabadiliko ya uwekaji kama sehemu ya marekebisho ya mpango wa usaidizi wa tabia.

### Hali maalum

Iwe tabia hiyo ilikuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto wako au la, wafanyakazi wa shule wanaweza kumwondoa mwanafunzi na kumweka katika mazingira mbadala ya elimu ya muda (yalioamuliwa na Timu ya IEP ya mtoto) kwa kipindi kisichozidi siku 45 za shule, ikiwa mtoto wako:

1. Ataleta silaha (tazama ufafanuzi hapa chini) shuleni au ana silaha shuleni, kwenye majengo ya shule, au katika tukio la shule chini ya mamlaka ya Shirika la Elimu la Jimbo au wilaya ya shule;
2. Kwa kujua ana au hutumia dawa haramu za kulevya (tazama ufafanuzi hapa chini), au anauza au kuomba uuzaji wa dawa inayodhibitiwa, (tazama ufafanuzi hapa chini), akiwa shuleni, kwenye majengo ya shule, au katika tukio la shule chini ya mamlaka ya Shirika la Elimu la Jimbo au wilaya ya shule; **au**

3. Amesababisha jeraha baya la mwili (tazama ufafanuzi hapa chini) kwa mtu mwingine akiwa shuleni, kwenye majengo ya shule, au katika tukio la shule chini ya mamlaka ya Shirika la Elimu la Jimbo au wilaya ya shule.

**Ufafanuzi**

*Dawa inayodhibitiwa* inamaanisha dawa au dutu nyingine iliyotambuliwa chini ya ratiba za I, II, III, IV, au V katika sehemu ya 202 (c) ya Sheria ya Udhibiti wa Dawa (21 U.S.C. 812 (c)).

*Dawa haramu* inamaanisha dawa inayodhibitiwa; lakini haijumuishi dawa inayodhibitiwa ambayo inamilikiwa kihalali au kutumika chini ya usimamizi wa mtaalamu wa huduma za afya aliye na leseni au ambayo inamilikiwa kihalali au kutumika chini ya mamlaka nyingine yoyote chini ya Sheria hiyo au chini ya kifungu kingine chochote cha sheria ya Shirikisho.

*Jeraha baya la mwili* linamaanisha ufafanuzi uliotolewa kwa istilahi ‘‘jeraha baya la mwili’ chini ya aya ya (3) ya sehemu ndogo ya (h) ya sehemu ya 1365 ya kichwa cha 18, Kanuni ya Marekani.

*Silaha* inamaanisha ufafanuzi uliotolewa kwa maneno ‘‘silaha hatari’’ chini ya aya ya (2) ya sehemu ndogo ya kwanza ya (g) ya sehemu ya 930 ya kichwa cha 18, Kanuni ya Marekani.

**Taarifa**

Katika tarehe inapofanya uamuzi wa kuondolewa ambao ni mabadiliko ya uwekaji wa mtoto wako kwa sababu ya ukiukaji wa kanuni ya maadili mema ya mwanafunzi, wilaya ya shule lazima ikujulishe kuhusu uamuzi huo, na ikupe notisi ya ulinzi wa utaratibu.

# MABADILIKO YA UWEKAJI KWA SABABU YA UONDOAJI WA KINIDHAMU

## 34 CFR § 300.536

Kuondolewa kwa mtoto wako mwenye ulemavu kutoka kwa uwekaji wa sasa wa elimu ya mtoto wako ni **mabadiliko ya uwekaji** ikiwa:

1. Kuondolewa kunazidi siku 10 za shule za mfululizo; **au**
2. Mtoto wako amekabiliwa na uondoaji wa mfululizo ambao umekuwa mtindo kwa sababu:
    a. Uondoaji wa mfululizo una jumla ya siku 10 za shule katika mwaka wa shule;
    b. Tabia ya mtoto wako ni sawa kwa kiwango kikubwa na tabia ya mtoto katika matukio ya awali ambayo yalisababisha uondoaji wa mfululizo; na
    c. Sababu za ziada kama vile urefu wa kila uondoaji, jumla ya muda ambao mtoto wako ameondolewa, na ukaribu kati ya vipindi vya uondoaji.

Uamuzi wa iwapo mtindo wa kuondolewa unajumuisha mabadiliko ya uwekaji huamuliwa kwa msingi wa kila kisa na wilaya ya shule na, ikiwa unapingwa, unapaswa kukaguliwa kupitia mchakato wa haki na kesi za mahakama.

# UBAINISHAJI WA MAZINGIRA

## 34 CFR § 300.531

Timu ya Mpango wa Elimu Binafsi (IEP) huamua mazingira mbadala ya elimu ya muda kwa hatua za kuondolewa ambazo ni **mabadiliko ya uwekaji**, na hatua za kuondolewa chini ya vichwa vidogo vya ***Mamlaka ya ziada*** na ***Hali maalum***.

# RUFAA

## 34 CFR § 300.532

### Jumla

Unaweza kuwasilisha lalamiko la mchakato wa haki (tazama kichwa cha ***Taratibu za Lalamiko la Mchakato wa Haki***) ili kuomba usikiliaji wa kesi ya mchakato wa haki ikiwa haukubaliani na:

1. Uamuzi wowote kuhusu uwekaji uliotolewa chini ya masharti haya ya nidhamu; **au**
2. Ubainishaji wa udhihirisho ulioelezwa hapo juu.

Wilaya ya shule inaweza kuwasilisha lalamiko la mchakato wa haki (tazama hapo juu) ili kuomba usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki ikiwa inaamini kuwa kudumisha uwekaji wa sasa wa mtoto wako kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha kuumia kwa mtoto wako au wengine.

### Mamlaka ya hakimu

Hakimu anayekidhi masharti yaliyoelezwa chini ya kichwa kidogo cha ***Hakimu asiye na upendeleo*** lazima aandae usikilizaji wa kesi ya mchakato wa haki na afanye uamuzi. Hakimu anaweza:

1. Kumrudisha mtoto wako mwenye ulemavu kwenye uwekaji ambao mtoto wako aliondolewa ikiwa hakimu ataamua kuwa kuondolewa kwa mtoto huyo kulikuwa ukiukaji wa masharti yaliyoelezwa chini ya ***Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule***, au kwamba tabia ya mtoto wako ilikuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto wako; **au**
2. Kuagiza mabadiliko ya uwekaji wa mtoto wako mwenye ulemavu kwa mazingira mbadala yanayofaa ya elimu ya muda, kwa muda usiozidi siku 45 za shule ikiwa hakimu ataamua kuwa kudumisha uwekaji wa sasa wa mtoto wako kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha kuumia kwa mtoto wako au wengine.

Taratibu hizi za usikilizaji wa kesi zinaweza kurudiwa, ikiwa wilaya ya shule inaamini kuwa kumrudisha mtoto wako kwenye uwekaji wa awali kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha kuumia kwa mtoto wako au wengine.

Wakati wowote wewe au wilaya ya shule inapowasilisha lalamiko la mchakato wa haki ili kuomba usikilizaji kama huo wa kesi, usikilizaji lazima uandaliwe ambao unakidhi masharti yaliyoelezwa chini ya vichwa vya ***Taratibu za Lalamiko la Mchakato wa Haki, Usikilizaji wa Kesi za Malalamiko ya Mchakato wa Haki*** isipokuwa ifuatavyo:

1. Shirika la Elimu la Jimbo au wilaya ya shule lazima ipange usikilizaji wa haraka wa kesi ya mchakato wa haki, ambao lazima ufanyike ndani ya siku **20** za shule kuanzia tarehe ambayo usikilizaji huo wa kesi uliombwa na lazima itoe uamuzi ndani ya siku **10** za shule baada ya kikao cha usikilizaji.
2. Isipokuwa wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kwa maandishi kuondoa mkutano, au mnakubaliana kutumia upatanisho, mkutano wa utatuzi lazima ufanyike ndani ya siku **saba** za kalenda baada ya kupokea notisi ya lalamiko la mchakato wa haki. Usikilizaji wa kesi unaweza kuendelea isipokuwa suala hilo limetatuliwa kwa njia inayoridhisha pande zote mbili ndani ya **15** za kalenda baada ya kupokea lalamiko la mchakato wa haki.
3. Jimbo linaweza kuweka kanuni tofauti za utaratibu kwa ajili ya kuharakisha vikao vya kesi za mchakato wa haki kuliko ilizoweka kwa vikao vingine vya kesi za mchakato wa haki, lakini isipokuwa kwa ratiba, kanuni hizo lazima ziendane na kanuni zilizo katika hati hii kuhusu vikao vya usikilizaji wa kesi za mchakato wa haki.

Wewe au wilaya ya shule inaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi uliofanywa katika usikilizaji wa haraka wa kesi za mchakato wa haki kwa njia sawa na maamuzi katika vikao vingine vya kesi za mchakato wa haki (tazama kichwa cha ***Rufaa***).

# UWEKAJI WAKATI WA RUFAA

## 34 CFR § 300.533

Wakati, kama ilivyoelezwa hapo juu, wewe au wilaya ya shule itawasilisha lalamiko la mchakato wa haki kuhusiana na masuala ya nidhamu, mtoto wako lazima (isipokuwa wewe na Shirika la Elimu la Jimbo au wilaya ya shule mkubaliane vinginevyo) abaki katika mazingira mbadala ya elimu ya muda akisubiri uamuzi wa hakimu, au mpaka muda wa kuondolewa ukimalizika kama ilivyobainishwa na ilivyoelezwa chini ya kichwa cha ***Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule***, chochote kinachotokea kwanza.

# ULINZI KWA WATOTO AMBAO BADO HAWAJASTAHIKI ELIMU MAALUM NA HUDUMA ZINAZOHUSIANA

## 34 CFR § 300.534

### Jumla

Ikiwa mtoto wako hajabainishwa kuwa anastahiki elimu maalum na huduma zinazohusiana na akiuke kanuni ya maadili mema ya mwanafunzi, lakini wilaya ya shule ilifahamu (kama ilivyobainishwa hapo chini) kabla ya kutokea kwa tabia iliyosababisha hatua za kinidhamu, kwamba mtoto wako alikuwa mtoto

mwenye ulemavu, basi mtoto wako anaweza kudai ulinzi wowote ulioelezwa katika notisi hii.

### Msingi wa ufahamu kwa masuala ya nidhamu

Wilaya ya shule itachukuliwa kuwa na ufahamu kwamba mtoto wako ni mtoto mwenye ulemavu ikiwa, kabla ya kutokea kwa tabia iliyosababisha hatua ya kinidhamu:

1. Ulielezea wasiwasi kwa maandishi kwa wasimamizi au wafanyakazi wa utawala wa shirika linalofaa la kielimu, au kwa mwalimu wa mtoto wako kwamba mtoto wako anahitaji elimu maalum na huduma zinazohusiana;
2. Uliomba tathmini inayohusiana na ustahiki wa elimu maalum na huduma zinazohusiana chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA; **au**
3. Mwalimu wa mtoto wako au mfanyakazi mwingine wa wilaya ya shule alieleza wasiwasi mahususi kuhusu mtindo wa tabia ya mtoto wako moja kwa moja kwa mkurugenzi wa elimu maalum wa wilaya ya shule au kwa wafanyakazi wengine wa usimamizi wa wilaya ya shule.

### Hali za kipekee

Wilaya ya shule haitachukuliwa kuwa na ufahamu huo ikiwa:

1. Hujaruhusu tathmini ya mtoto wako au umekataa huduma za elimu maalum; **au**
2. Mtoto wako ametathminiwa na kubainishwa kuwa mtoto asiye na ulemavu chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA.

### Masharti yanayotumika ikiwa hakuna msingi wa ufahamu

Ikiwa kabla ya kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mtoto wako, wilaya ya shule haina ufahamu kwamba mtoto wako ni mtoto mwenye ulemavu, kama ilivyoelezwa hapo juu chini ya vichwa vidogo vya ***Msingi wa ufahamu wa masuala ya nidhamu*** na ***Hali za kipekee***, mtoto wako anaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu ambazo zinatumika kwa watoto wasio na ulemavu ambao wanajihusisha na tabia zinazofanana.

Hata hivyo, ikiwa utatuma ombi la tathmini ya mtoto wako wakati wa kipindi ambacho mtoto wako anachukuliwa hatua za kinidhamu, tathmini lazima ifanywe kwa njia ya haraka.

Hadi tathmini itakapokamilika, mtoto wako hubaki katika uwekaji wa elimu ulioamuliwa na mamlaka ya shule, ambao unaweza kujumuisha kusimamishwa au kufukuzwa shuleni bila kupewa huduma za elimu.

Ikiwa mtoto wako amebainishwa kuwa mtoto mwenye ulemavu, kwa kuzingatia taarifa kutoka kwa tathmini iliyofanywa na wilaya ya shule, na taarifa zilizotolewa na wewe, wilaya ya shule lazima itoe elimu maalum na huduma zinazohusiana kulingana na Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, ikiwa ni pamoja na masharti ya nidhamu yaliyoelezwa hapo juu.

# RUFAA KWA, NA HATUA YA MAMLAKA ZA UTEKELEZAJI WA SHERIA NA MAMLAKA ZA MAHAKAMA

## 34 CFR § 300.535

Sehemu ya B ya sheria ya IDEA haijumuishi:

1. Kuzuia shirika kuripoti uhalifu uliofanywa na mtoto mwenye ulemavu kwa mamlaka husika; **au**
2. Kuzuia mamlaka za utekelezaji wa sheria na mamlaka za mahakama za Jimbo kutekeleza majukumu yao kuhusiana na matumizi ya sheria ya Shirikisho na Jimbo kwa uhalifu uliofanywa na mtoto mwenye ulemavu.

### Utumaji wa rekodi

Ikiwa wilaya ya shule itaripoti uhalifu uliofanywa na mtoto mwenye ulemavu, wilaya ya shule:

1. Lazima ihakikishe kwamba nakala za elimu maalum na rekodi za nidhamu za mtoto zinatumwa ili kuzingatiwa na mamlaka ambako shirika linaripoti uhalifu; **na**
2. Inaweza kutuma nakala za elimu maalum na rekodi za nidhamu za mtoto wako kwa kiwango tu kinachoruhusiwa na Sheria ya Haki za Elimu za Familia na Faragha (FERPA).

# MASHARTI YA UAMUZI WA WAZAZI WA KUWEKA WATOTO KATIKA SHULE ZA KIBINAFSI KWA GHARAMA ZA SERIKALI

## JUMLA

## 34 CFR § 300.148

Sehemu ya B ya sheria ya IDEA haihitaji wilaya ya shule kulipia gharama za elimu, ikiwa ni pamoja na elimu maalum na huduma zinazohusiana, za mtoto wako mwenye ulemavu katika shule au kituo cha kibinafsi ikiwa wilaya ya shule ilitoa elimu ya bure na inayofaa ya umma (FAPE) kwa mtoto wako na ukachagua kumweka mtoto katika shule au kituo cha kibinafsi. Hata hivyo, wilaya ya shule ambapo shule ya kibinafsi inapatikana lazima ijumuishe mtoto wako miongoni mwa watu ambao mahitaji yao yanashughulikiwa chini ya masharti ya Sehemu ya B kuhusu watoto ambao wamewekwa na wazazi wao katika shule ya kibinafsi chini ya 34 CFR § 300.131 hadi 300.144.

### Urejeshaji wa malipo kwa ajili ya uwekaji katika shule ya kibinafsi

Ikiwa mtoto wako hapo awali alipokea elimu maalum na huduma zinazohusiana chini ya mamlaka ya wilaya ya shule, na unachagua kuandikisha mtoto wako katika shule ya kibinafsi ya chekechea, ya msingi, au ya sekondari bila idhini au rufaa ya wilaya ya shule, mahakama au hakimu anaweza kuhitaji shirika kukurejeshea gharama ya uandikishaji huo ikiwa mahakama au hakimu atabaini kuwa shirika halikuwa limetoa elimu ya bure na inayofaa ya umma (FAPE) kwa mtoto wako kwa wakati unaofaa kabla ya uandikishaji huo na kwamba uwekaji katika shule ya kibinafsi unafaa. Hakimu au mahakama inaweza kubaini kuwa uwekaji wako ulifaa, hata kama uwekaji haukidhi viwango vya Jimbo vinavyotumika kwa elimu inayotolewa na Shirika la Elimu la Jimbo na wilaya za shule.

### Vikomo vya urejeshaji wa malipo

Gharama ya urejeshaji iliyoelezwa katika aya iliyo hapo juu inaweza kupunguzwa au kukataliwa:

1. Ikiwa: (a) Katika mkutano wa hivi karibuni wa mpango wa elimu binafsi (IEP) ambao ulihudhuria kabla ya kuondolewa kwa mtoto wako kutoka shule ya umma, hukujulisha Timu ya IEP kwamba ulikuwa unakataa uwekaji uliopendekezwa na wilaya ya shule wa kumpa mtoto wako FAPE, ikiwa ni pamoja na kueleza wasiwasi wako na nia yako ya kuandikisha mtoto wako katika shule ya kibinafsi kwa gharama ya serikali; au (b) Angalau siku 10 za kazi (ikiwa ni pamoja na sikukuu yoyote ambayo hutokea katika siku ya kazi) kabla ya kuondolewa kwa mtoto wako kutoka shule ya umma, hukutoa notisi ya maandishi kwa wilaya ya shule ya taarifa hiyo;
2. Ikiwa, kabla ya kuondolewa kwa mtoto wako kutoka shule ya umma, wilaya ya shule ilikupatia notisi ya awali iliyoandikwa kuhusu nia yake ya kutathmini mtoto wako (ikiwa ni pamoja na taarifa ya madhumuni ya kufanya tathmini hiyo ambayo yalikuwa yanafaa na ya kutosha), lakini hukumfanya mtoto apatikane kwa tathmini hiyo; **au**
3. Baada ya mahakama kubaini kwamba matendo yako hayakuwa ya busara.

Hata hivyo, gharama ya urejeshaji:

1. Haipaswi kupunguzwa au kukataliwa kwa kukosa kutoa notisi ikiwa: (a) Shule ilikuzuia kutoa notisi hiyo; (b) Hukuwa umepokea notisi ya wajibu wako wa kutoa notisi iliyoelezwa hapo juu; au (c) Kufuata masharti ya hapo juu kunaweza kusababisha madhara ya kimwili kwa mtoto wako; **na**

2. Haipaswi, kwa hiari ya mahakama au afisa wa kusikiliza, kupunguzwa au kukataliwa kwa kukosa kwako kutoa notisi inayohitajika ikiwa: (a) Hujui kusoma au kuandika kwa Kiingereza; au (b) Kufuata masharti yaliyo hapo juu kunaweza kusababisha madhara makubwa ya kihisia kwa mtoto wako.

## Ufafanuzi wa Siku na Aina ya "Siku"

"Siku" inafafanuliwa katika Sehemu ya 300.9 ya sheria ya IDEA kama:

(a) **Siku** inamaanisha siku ya kalenda isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo kama siku ya kazi au siku ya shule;

(b) **Siku ya kazi** inamaanisha Jumatatu hadi Ijumaa, isipokuwa kwa sikukuu za Shirikisho na Jimbo (isipokuwa ikiwa sikukuu hizo hasa zimejumuishwa katika siku ya kazi, kulingana na Sehemu ya 300.403(d)(1)(ii); na

(c) (1) **Siku ya shule** inamaanisha siku yoyote, ikiwa ni pamoja na siku ambayo watoto wanahudhuria shule kwa muda mahususi kwa madhumuni ya kufundishwa

## KIMBATISHO CHA A:
## Taarifa iliyoandikwa Kuhusu Matumizi ya Msaada au Bima ya Serikali

**TAARIFA ILIYOANDIKWA KUHUSU MATUMIZI YA MSAADA AU BIMA YA SERIKALI**

Mpendwa Mzazi au Mlezi:

Unapokea taarifa hii iliyoandikwa ili kukupa habari kuhusu haki zako na ulinzi chini ya sheria ya elimu maalum ya shirikisho, Sheria ya Elimu ya Watu wenye Ulemavu (IDEA), kuhusu matumizi ya msaada na bima ya serikali kwa mtoto wako. Katika New Hampshire "msaada na bima ya serikali" ni Medicaid, ambayo hutolewa kupitia mpango wa Jimbo wa Medicaid kwa Shule (Medicaid to Schools), ikiwa ni pamoja na mipango ya Medicaid inayotolewa kupitia shirika la huduma inayodhibitiwa. Kupitia Mpango wa Medicaid kwa Shule, wilaya za shule za NH katika jimbo zima hupokea mamilioni ya dola kila mwaka ambayo vinginevyo yangetoka kwa vyanzo vya fedha vya Jimbo au eneo.

Fedha za IDEA hulipia sehemu ya elimu maalum na huduma zinazohusiana za mtoto wako. Fedha kutoka kwa mpango wa msaada au bima ya serikali, ambao katika NH ni Medicaid, pia zinaweza kutumiwa na wilaya yako ya shule kusaidia kulipia elimu maalum na huduma zinazohusiana kulingana na IEP ya mtoto wako, lakini ikiwa tu utachagua kutoa idhini yako. Wilaya yako ya shule haiwezi kufikia msaada wa Medicaid wa mtoto wako ikiwa utakusababishia gharama, kama vile kupunguzwa kwa msaada wako au ongezeko la malipo yako.

Wilaya ya shule ina jukumu la kuhakikisha kuwa mtoto wako anapata huduma zote zilizo katika IEP yake, bila kujali kama unatoa idhini kwa wilaya ya shule kutumia msaada au bima ya serikali kwa mtoto wako. Ikiwa hutatoa idhini, au ukiondoa idhini yako baada ya kuitoa, huduma za mtoto wako hazitaathiriwa; huduma zote zilizo katika IEP ya mtoto wako zitaendelea kutolewa. Pia huhitajiki kutuma ombi la au kumwandikisha mtoto wako katika mpango wa Medicaid ili apokee huduma za elimu maalum.

**WAKATI AMBAPO TAARIFA ILIYOANDIKWA LAZIMA ITOLEWE**

Kabla ya wilaya yako ya shule kukuomba utoe idhini yako ya kufikia Medicaid ya mtoto wako kwa mara ya kwanza, lazima ikupe taarifa hii ya haki na ulinzi unaopatikana kwako chini ya sheria ya IDEA.

- Sheria ya IDEA inahitaji kwamba upewe notisi hii kabla ya wilaya ya shule kunuia kutumia Medicaid ya mtoto wako kwa mara ya kwanza,
- Kabla ya kupata idhini yako ya kutumia msaada huo kwa mara ya kwanza; **na**
- Kila mwaka baada ya hapo.

Taarifa hii iliyoandikwa lazima iwe imeandikwa katika lugha inayoeleweka kwa umma na katika lugha yako ya asili au katika njia nyingine ya mawasiliano unayotumia, isipokuwa kama haiwezekani kufanya hivyo.

**IDHINI YA MZAZI**

Kabla ya wilaya yako ya shule kutumia msaada au bima ya serikali ya mtoto wako kwa mara ya kwanza kulipia elimu maalum na huduma zinazohusiana chini ya sheria ya IDEA, lazima ipate idhini yako iliyosainiwa na iliyoandikwa tarehe. Wilaya yako ya shule itakupa fomu ya idhini ambayo utasaini na kuandika tarehe. Wilaya yako ya shule inahitajika tu kupata idhini yako *mara* moja.

Masharti ya idhini yana sehemu mbili:

1) Idhini ya kufichua taarifa binafsi inayoweza kutambulisha ya mtoto wako kwa shirika la jimbo linalowajibika kutoa Medicaid.
   - Ili kufikia Medicaid ya mtoto wako, taarifa fulani ya binafsi inayoweza kutambulisha mtu itafichuliwa kwa madhumuni ya wilaya ya shule kutuma bili kwa shirika la Jimbo la Medicaid au wakala wa bili wa Medicaid. Chini ya sheria ya shirikisho, idhini yako ya maandishi inahitajika kabla ya wilaya ya shule kufichua taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha mtu (kama vile jina la mtoto wako, anwani, nambari ya mwanafunzi, IEP, au matokeo ya tathmini) kutoka kwa rekodi za elimu za mtoto wako kwa mhusika mwingine isipokuwa wilaya yako ya shule, isipokuwa ikiwa kuna hali za kipekee. Idhini yako ya kwanza, ya matumizi ya Medicaid ya mtoto wako, inaruhusu wilaya yako ya shule kufichua taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha mtu, zinazohitajika kwa ajili ya malipo ya Medicaid, kwa shirika la Jimbo la Medicaid au wakala wa bili wa Medicaid.

2) Taarifa ya kufikia Medicaid ya mtoto wako:
   - Idhini yako inayoruhusu wilaya ya shule kutumia Medicaid ya mtoto wako haitakugharimu chochote, na haitakuwa na athari mbaya kwa huduma zingine zozote muhimu za matibabu ambazo mtoto wako anaweza kupokea kupitia mfumo wa Medicaid. Kuna ulinzi maalum kuhusu matumizi ya Medicaid:
     - Wilaya ya shule lazima ipate idhini ya mzazi iliyoandikwa kabla ya kutumia Medicaid ya mtoto wako kwa mara ya kwanza.
     - Wilaya yako ya shule haiwezi kufikia (kutumia) Medicaid ya mtoto wako ikiwa matumizi hayo:
       - Yatapunguza bima ya maisha au msaada mwingine wowote unaopatikana wa Medicaid;
       - Yatasababisha familia kulipia huduma muhimu za matibabu (iwe zimetolewa shuleni au katika mazingira mengine) ambazo vinginevyo zinalipiwa na Medicaid ya mtoto.
       - Yataongeza malipo (ikiwa yanalipwa) au kusababisha kusitishwa kwa msaada au bima; au
       - Yatasababisha hatari ya kupoteza ustahiki wa maondoleo ya masharti ya kawaida yanayotumika kwa huduma za nyumbani na jamii, kulingana na matumizi ya jumla yanayohusiana na afya.

**UONDOAJI WA IDHINI**

- Ikiwa ulitoa idhini yako kwa wilaya yako ya shule kufichua taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha za mtoto wako kwa shirika la Jimbo ambalo lina jukumu la kusimamia Medicaid ya mtoto wako, una haki chini ya sheria ya shirikisho kuondoa idhini hiyo wakati <u>wowote.</u>
- Ikiwa hutaki wilaya yako ya shule kuendelea kutoza mpango wako au wa mtoto wako wa msaada au bima ya serikali kwa elimu maalum na huduma zinazohusiana chini ya sheria IDEA, utahitaji kuondoa idhini yako ambayo inaruhusu wilaya ya shule kupata msaada wa Medicaid ya mtoto wako. Kwa kuondoa idhini yako, unakomesha ruhusa ya mamlaka ya wilaya ya shule kufikia mpango wa msaada au bima wa Jimbo wa mtoto wako. Uondoaji huu wa idhini unatumika kuanzia wakati ambapo wilaya ya shule inapokea hati uliyosaini ya uondoaji wa idhini.

*Jaza sehemu iliyo hapa chini* <u>*TU*</u> *ikiwa mzazi/mlezi anaondoa idhini ya kufikia Medicaid ya mtoto.*

**<u>UONDOAJI WA IDHINI</u>**

Jina la Mwanafunzi: _____________________________________ Tarehe ya Kuzaliwa______/_______/______

Nambari ya Kitambulisho cha Medicaid_______________________________________

Kama mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliye hapo juu, ninaondoa idhini yangu ya kuruhusu wilaya ya shule kufikia Medicaid ya mtoto. Ninaelewa kuwa hii inamaanisha kuwa wilaya ya shule haitaweza tena kutumia Medicaid ya mtoto wangu kusaidia kulipia elimu maalum na huduma zinazohusiana za mtoto wangu. Uondoaji wa idhini unaanza kutumika kuanzia wakati wilaya ya shule inapopokea fomu iliyosainiwa na mzazi/mlezi ya *Uondoaji wa Idhini*.

__________________________________________ _____________________________
Saini ya Mzazi Tarehe ya Leo

*Hifadhi hati halisi kwenye faili ya mwanafunzi -----tuma nakala kwa mzazi/mlezi*